Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Arobaini na Mbili - Tarehe 6 Agosti, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED - MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI *(PAC):***

Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali *(PAC)* kuhusu Uchunguzi wa Matumizi ya Fedha na Taratibu za Utendaji Kazi *TVT, TACAIDS,* Kitengo cha Maafa, *Tansort* na *London Trade Centre (LTC).*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 395

**Magari ya Kubebea Wagonjwa Kwenye Hospitali za Wilaya**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa magari ya kubeba wagonjwa *(Ambulance)* ni muhimu sana na kwa kuwa zipo Hospitali za Wilaya ambazo hazina magari ya kubeba wagonjwa hapa nchini:-

(a) Je, ni Hospitali za Wilaya ngapi ambazo zina magari ya kubebea wagonjwa hapa nchini?

(b) Kwa Hospitali za Wilaya ambazo hazina magari ya aina hiyo ikiwemo Hospitali ya Wilaya ya Mpwapwa, je, Serikali ina mpango gani wa kuzipatia magari ili yaweze kutoa huduma katika Wilaya hizo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inalifahamu tatizo la uhaba wa magari ya kubebea wagonjwa linalozikabili Hospitali nyingi za Wilaya na Vituo vya Afya hapa nchini. Hali hii inafanya usafirishaji wa haraka kwa wagonjwa wa rufaa *(referral cases)* kuwa mgumu.

Mheshimiwa Spika, kati ya Wilaya za kiutawala 106 zilizopo, Wilaya 75 tu ndizo zilizo na Hospitali kamili. Wilaya 20 zinatumia Hospitali Teule *(Designated Hospitals)* na zilipo Makao Makuu ya Mikoa zinatumia Hospitali za Mikoa.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoelezea katika hotuba ya Bajeti ya mwaka 2003/2004 na 2004/2005, Ofisi yangu imekuwa inaendelea na juhudi za kutenga fedha kwa ajili ya kununua magari ya kubebea wagonjwa katika Vituo vya Afya na Hospitali za Wilaya zote. Azma hii ya Serikali inatekelezwa polepole kutokana na ufinyu wa bajeti. Hata hivyo, Serikali inaendelea kuzishauri Halmashauri za Wilaya kutoa kipaumbele cha ununuzi wa magari ya wagonjwa ya Hospitali zao za Wilaya na Vituo vya Afya katika makadirio ya mipango yao ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kumwarifu Mheshimiwa George Lubeleje, kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa kwa mwaka huu wa fedha 2004/2005 imetenga shilingi milioni 50 kwa ajili ya kununulia gari la wagonjwa.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali la nyongeza.

Kwa kuwa tatizo hili ni la muda mrefu na kwa kuwa kuna wananchi ambao wanapoteza maisha yao kwa sababu wanakosa usafiri wa kufika hospitali mapema, je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba ipo haja sasa kuweka mikakati ili kumaliza tatizo hili katika nchi yetu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge na kwa kweli Serikali inao mkakati wa kupatia magari vituo vyote vya Afya na Hospitali za Wilaya. Lakini hili siyo jukumu la Serikali Kuu peke yake ni jukumu vile vile la Halmashauri zote za Wilaya, zinatakiwa zijipangie katika bajeti zao fedha kwa ajili ya ununuzi wa magari haya, zisitegemee ruzuku za Serikali peke yake.

**MHE. NJELU E.M. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa katika jibu lake la msingi alipokuwa anajibu habari za Hospitali ya Mpwapwa amesema kuna Wilaya ambazo wana hospitali ambazo ni *DDH* yaani walizoziazima kutoka

mashirika mengine, je, nilitaka kujua hili suala la kuwa na hospitali za *DDH* ni la kudumu au limekuwa la mpito hatimaye hizo Wilaya ambazo hazina hospitali kama Wilaya ya Chunya ziweze kuwa na Hospitali za Serikali?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuwa na hospitali za *DDH* ni wa muda na ni wa kupita mara Serikali itakapokuwa na uwezo wa kuwa na hospitali za Wilaya zitajengwa. Lakini napenda kusisitiza tena kwamba, jukumu la kuandaa na kujenga zahanati, vituo vya afya na hospitali za Wilaya ni jukumu la Halmashauri, Serikali itachangia na kuongeza nguvu pale inapowezekana. Kwa hiyo, kwa Wilaya na Halmashauri ambazo hazina hospitali za Wilaya, tunazishauri zianze nazo kujiwekea utaratibu wa kujiwezesha kujenga hospitali hizo na Serikali itasaidia.

Na. 396

**Hali ya Uwekezaji Nchini**

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO** aliuliza:-

Kwa kuwa Sheria ya Kituo cha Uwekezaji, *Tanzania Investment Centre (TIC)* ilirekebishwa kwa lengo la kuondoa dosari zilizokuwepo katika sheria ya awali na hivyo kuboresha mazingira ya uwekezaji hapa nchini:-

(a) Baada ya kuondoa dosari katika sheria iliyokuwepo, je, *TIC* imekuwa *one stop centre* sawasawa na humchukua mwekezaji kutoka nje muda gani kuweza kupata uamuzi wa kuwekeza?

(b) Je, uwekezaji umekua kwa kiasi gani baada ya sheria hiyo kufanyiwa marekebisho katika sehemu za Kilimo, Viwanda, Madini, Usafirishaji (Ardhini, Majini na Angani), Utalii na huduma za Hoteli, Nishati, Biashara ya Mafuta *(Petroleum)* na Mawasiliano *(Telecommunication)?*

(c) Je, wawekezaji kutoka nje ya nchi wanawajibika kulipa kodi gani pindi waamuapo kuuza Kampuni zao kwa wamiliki wengine wa nje?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, baada ya kupitishwa kwa Sheria mpya ya Uwekezaji katika mfumo wa *One stop Centre,* Kituo cha Uwekezaji Rasilimali kimeweza kutoa huduma kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kwa urahisi na kwa ufanisi mkubwa. Idadi ya miradi iliyosajiliwa ilifikia miradi 372 mwaka 2003 ikilinganishwa na miradi 111 mwaka 1996. Pia viwango vya mitaji *(investments)* ilifikia shilingi milioni

1,669,369 mwaka 2003 ikilinganishwa na shilingi milioni 376,980 kwa mwaka 1996. Kituo kinatumia muda wa siku kumi na nne kushughulikia maombi ya mwekezaji kuanzia siku anayowasilisha maombi hadi kutolewa kwa *Certificate of Incentives.* Takwimu hizi zinaonyesha kuongezea kwa kasi ya uwekezaji nchini baada ya kuanza kutumika kwa mfumo wa *One Stop Centre.*

(b) Mheshimiwa Spika, kwa ujumla kutokana na mipango mizuri kupitia *TIC,* uwekezaji umekua kwa kiwango kikubwa Takwimu kwa ukuaji wa uwekezaji kwa sekta alizouliza Mheshimiwa Mbunge ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sekta ya kilimo, idadi ya miradi iliyosajiliwa iliongezeka na kufikia miradi 20 mwaka 2003 ikilinganisha na miradi sita mwaka 1996 na viwango vya mitaji kufikia shilingi milioni 152,982 mwaka 2003 ikilinganishwa na shilingi milioni 4,206 mwaka 1996.

Mheshimiwa Spika, sekta ya viwanda, miradi 127 ilisajiliwa mwaka 2003 ikilinganishwa na miradi 65 mwaka 1996 na viwango vya mitaji kufikia shilingi milioni 239,622 mwaka 2003 ikilinganishwa na shilingi milioni 184,623 mwaka 1996.

Mheshimiwa Spika, sekta ya madini na petroli, miradi 19 ilisajiliwa mwaka 2002 ikilinganishwa na mradi mmoja mwaka 1996 na viwango vya mitaji kufikia shilingi milioni 38,969 mwaka 2003 ikilinganisha na shilingi milioni 4,680 mwaka 1996.

Sekta ya usafirishaji, miradi 28 ilisajiliwa mwaka 2003 ikilinganishwa na miradi sita mwaka 1996 na viwango vya mitaji kufikia shilingi milioni 80,935 mwaka 2003 ikilinganishwa na shilingi milioni 8,999 mwaka 1996.

Sekta ya utalii na huduma za hoteli, miradi 81 ilisajiliwa mwaka 2003 ikilinganishwa na miradi 12 mwaka 1996 na viwango vya mitaji kufikia shilingi milioni 127,157 mwaka 2003 ikilinganishwa na shilingi milioni 20,115 mwaka 1996.

Mheshimiwa Spika, sekta ya nishati, miradi minne ilisajiliwa mwaka 2002 ikilinganishwa na mradi mmoja mwaka 1996 na viwango vya mitaji kufikia shilingi milioni 605 mwaka 2002 ikilinganishwa na shilingi milioni 97,800 mwaka 1996.

Mheshimiwa Spika, sekta ya mawasiliano, miradi 12 ilisajiliwa mwaka 2003 ikilinganishwa na miradi miwili mwaka 1996 na viwango vya mitaji kufikia shilingi milioni 111,615 mwaka 2003 ikilinganishwa na shilingi milioni 8052 mwaka 2003.

(c) Mheshimiwa Spika, wawekezaji kutoka nje wanawajibika kulipa kodi zote wanapoamua kuuza Kampuni zao kwa wamiliki wengine wa nje. Kodi hizi ni pamoja na *Stamp Duty, Capital Gain Tax* kwa mujibu wa Sheria za Kodi hizi. Aidha, mwekezaji wa nje akiuza mali za kampuni ambazo zina msamaha wa kodi kwa kampuni ambayo haina *TIC Certificate of Incentives* itabidi mali hizo kulipwa kodi kwa mujibu wa sheria.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa swali hili linahusu uwekezaji, lakini pia linalenga kuhusu Pato la Tanzania. Takwimu zilizotolewa na Mheshimiwa Waziri zinaonyesha pato la jumla Tanzania imekuwa vizuri sana.

Sasa ni siri gani ambayo inasababisha Watanzania kwa kipato cha mtu mmoja mmoja kuonekana maskini? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba pato la jumla linakua, sasa kitu tunachokiangalia ni pato la mtu mmoja mmoja. Katika mipango yetu sisi tunavyoipanga, tumeanza kwanza na kupunguza umaskini usio wa kipato na ndio maana tunaendelea na taratibu za kujenga mashule, kuboresha maji, barabara na kadhalika. Tunakoelekea sasa ni kuangalia ni jinsi gani tutapunguza umaskini wa kipato na taratibu hizi tumeshazianza kwa miradi mbalimbali ambayo tumeelekeza kwenye sekta ya kilimo, lakini pamoja na hayo tuna hakika kabisa Sera ya Uwezeshaji tuliyoizindua katika Bunge hili itawezesha wananchi sasa kupata fursa za kuibua uchumi wao ili kuongeza kipato.

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri amesema inachukua siku kumi na nne kwa mradi kupitishwa na *TIC,* je, hicho ni kipimo kizuri cha ufanisi au kuna haja ya kuendelea kupunguza siku za kupitisha miradi hiyo pale *TIC?*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa viwango vya Tanzania hicho ni kipimo cha ufanisi mkubwa sana hasa tukizingatia kwamba wawekezaji mwanzoni walikuwa wanachukua kati ya miezi sita hata mwaka mmoja ili kupata *Certificate of Incentives* katika miradi yao.

Mheshimiwa Spika, lakini jitihada ambazo zinaendelea sasa hivi hasa za kuingiza utaalam wa *electronic,* tuna hakika kwamba siku hizo kumi na nne zitapungua na hata kufikia siku moja. *(Makofi)*

Na. 397

**Mfuko wa Kupambana na Umaskini**

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR (k.n.y. MHE. HAROUB SAID MASOUD)** aliuliza:-

Kwa kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais ndiyo inayosimamia Mfuko wa Kupambana na Umaskini ambao kwa kiasi fulani umesaidia sana baadhi ya Mikoa ya Tanzania Bara:-

(a) Je, ni Mikoa mingapi ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar imefaidika na Mfuko huo katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2003?

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha kilichosalia kwenye Mfuko huo katika kipindi hicho hicho?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mbunge wa Koani, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais inasimamia Mfuko wa Kutoa Mikopo Midogo Midigo *(Small Entrepreneurs Loan Facility - SELF)* ambao ulianzishwa kama jitihada mojawapo ya kupambana na umaskini nchini. Mradi huu hutoa mikopo kupitia asasi zinazohusika na utoaji mikopo kama *Pride, SIDO* na Vyama vya Kuweka na Kukopa *(SACCOS),* ambapo asasi hizi nazo hutoa mikopo hiyo kwa walengwa kwa ajili ya biashara ndogo ndogo ili kujiongezea kipato.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Haroub Said Masoud, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2003 Mikoa ambayo imenufaika na mradi wa *SELF* kwa Tanzania Bara ni Mtwara, Lindi, Dodoma, Morogoro, Singida, Pwani na Mikoa ya Tanzania Zanzibar. Mpaka kufikia mwishoni mwa Desamba, 2003 Wilaya zilizofikiwa na mradi ni Kibaha, Bagamoyo, Kisarawe, Rufiji na Mkuranga katika Mkoa wa Pwani, Lindi, Nachingwea na Kilwa, Mkoani Lindi, Masasi, Tandahimba na Newala katika Mkoa wa Mtwara na Wilaya za Kilosa, Mvomero na Morogoro. Wilaya nyingine ni Singida na Iramba, Dodoma, Kondoa, Mpwapwa na Kongwa na Unguja, Zanzibar.

Aidha, kwenye hotuba ya Ofisi ya Makamu wa Rais iliyopitishwa hapa Bungeni wiki iliyopita ilielezwa kuwa kuanzia mwaka huu wa fedha (2004/2005) Mikoa ifuatayo imeongezwa kwenye orodha ya walengwa ambayo ni Mbeya, Iringa, Ruvuma, Arusha, Tanga, Kilimanjaro, Mwanza na Mara.

(b) Mheshimiwa Spika, jumla ya shilingi milioni 955 ziliidhinishwa katika kipindi cha Januari - Desemba, 2003 kwa ajili ya mikopo. Kati ya hizo shilingi milioni 899 zilikopeshwa katika kipindi hicho na kiasi cha shilingi milioni 56 zilibaki. Jumla ya asasi za kifedha zipatazo 31 zilipatiwa mikopo.

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa Pemba ni Kisiwa maskini sana na wananchi wa Pemba wanajitahidi sana kufanya miradi mbalimbali wakiwemo wanawake na vijana, lakini hawana nyenzo na katika jibu lake Mheshimiwa Waziri hakutaja kama Mfuko huu umefika Pemba, kule Pemba tunausikia tu, je, Serikali sasa itakubaliana nami kwa udhati wake kwamba sasa ni wakati muafaka Mifuko hii kuja katika Kisiwa cha Pemba ili kusaidia wananchi kuondokana na umaskini? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO):** Mheshimiwa Spika, wakati nasimama sikuelewa ni nani,

lakini nilishauriwa kwamba kubali yaishe. Unapoambiwa kubali yaishe maana yake huna mpango na hilo jambo, lakini ningependa kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba labda kwa sababu tu sikueleweka, mpango huu wa *SELF* upo pia Tanzania Visiwani.

**WABUNGE FULANI:** Siyo Pemba, upo Unguja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO):** Kwa mfano, mwaka 2002 mpaka 2003, huko Pemba, asasi au *NGO* ya *Pride* ilikopa kutoka *SELF* na imewakopesha wananchi shilingi milioni 40 na Unguja kupitia asasi ya *Changamoto Life Preservation Fund,* mwaka 2001 walipata shilingi milioni 4, mwaka 2002/2003, walipata shilingi milioni 10 na mwaka 2003/2004, walipata shilingi milioni 40. *(Makofi)*

**MHE. KHAMIS AWESU ABOUD:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niulize swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize kama ifuatavyo:-

Kwa maelezo yake Mheshimiwa Waziri, alitueleza kuwa baadhi ya Mikoa na Wilaya imepangiwa mikopo hii maalum, je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa Mikoa yote itapata mikopo ili na wao wajijue kuwa wakifika kipindi fulani wamemaliza kupata hiyo mikopo yao? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO):** Mheshimiwa Spika, kama amenifuatilia vizuri na bila shaka amenifuatilia vizuri katika jibu langu. Tulianza na Mikoa michache na mwaka huu tumeongeza Mikoa mingine sita. Lengo letu kwa Mfuko huo ni kwamba tuendelee kuifikia Mikoa mingi zaidi na hatimaye Tanzania nzima.

Mheshimiwa Spika, labda kwa kumalizia ningeongeza hapa kwamba huo Mfuko wa *SELf* ni mmojawapo tu, tusisahau pia katika mkakati wa kuondoa umaskini mradi wa *TASAF* nao unalenga hivyo hivyo, pamoja na kuwapatia wananchi majengo na miradi mbalimbali lakini ndani yake kuna vile vile kuwawezesha kwa kuwapa posho wale ambao wanajishirikisha kwenye kazi za miradi ya *TASAF.* Kwa hiyo, huo nao pia ni mkakati mmojawapo wa kuondoa umaskini.

Na. 398

**Tathmini ya Hali ya Umaskini kwa Wanawake na Watoto**

**MHE. SEMINDU K. PAWA** aliuliza:-

Je, Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto imeshafanya tathmini yoyote juu ya:-

(a) Hali ya umaskini kwa wanawake wa Vijijini na Mijini?

(b) Hali ya watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu ili kuona kama hali hiyo inaongezeka au inapungua?

(c) Hali ya wanawake waliokopeshwa na baadhi ya Halmashauri ili kuona kama mikopo hiyo imewasaidia vipi na kwa kiwango gani?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Semindu Pawa, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama iufatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu haijafanya tathmini yoyote ya hali ya umaskini kwa wanawake Vijijini na Mijini. Hata hivyo zipo takwimu za mwaka 2000/2001 ambazo zimepatikana kupitia mfumo wa ufuatiliaji wa hali ya umaskini *(Poverty Monitoring System)* ambao upo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Utafiti uliofanywa kuhusu hali ya umaskini katika mapato na matumizi ya kaya binafsi *(Household Budget Survey)* kwa Tanzania Bara umeonyesha kuwa:-

- Kiwango cha umaskini kwa jamii zinazoishi Vijijini wakiwemo wanawake kinashuka taratibu ukilinganisha na kiwango cha umaskini kinavyoshuka Mijini.

- Wanawake wana kipato kidogo kuliko wanaume, ingawaje ni vigumu kupima tofauti katika matumizi kati ya mtu na mtu.

- Kumekuwepo na ongezeko kubwa la kaya zinazoongozwa na wanawake kuanzia asilimia 18 katika mwaka wa 1991/1992 hadi 33 katika mwaka 2002. Ingawaje sio maskini ikilinganishwa na kaya zinazoongozwa na wanaume.

- Wawake watu wazima wana kiwango kidogo cha elimu kuliko wanaume watu wazima.

(b) Mheshimiwa Spika, hali ya watoto wanaoishi katika mazingira magumu bado haijawa ya kuridhisha. Kutokana na tafiti zilizofanywa na wadau kama vile Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Shirika la Kuhudumia Watoto *(UNICEF),* Shirika la *AXIOS Foundation, TAMWA, KULEANA* na *Save the Children,* zinaonyesha kwamba kuna ongezeko la watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu. Hali hiyo inasababishwa na sababu mbalimbali zikiwemo za kiuchumi, kijamii, (mifarakano katika familia), kiutamaduni na ugonjwa wa UKIMWI ambapo kuna ongezeko la watoto yatima.

(c) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imefanya ufuatiliaji wa uendeshaji wa Mfuko huo wa *WDF* hususan katika utoaji wa mikopo na marejesho ili Mfuko huu uwe endelevu. Baada ya ufuatiliaji huo, tumebaini mabadiliko ya hali ya wanawake kama ifuatavyo:-

- Wanawake wa Mijini na Vijijini wamepata mwamko zaidi wa kufanya biashara.

- Baadhi ya wanawake wanajitegemea na wameweza kutatua matatizo yao kama vile kuchangia gharama za kuwaelimisha watoto wao, kununua nguo, kuchangia huduma za matibabu na kuwa na akaunti za akiba katika benki.

- Wanawake waliopata mikopo hiyo wameweza kushiriki katika Maonesho ya Biashara ya Kimataifa yanayofanyika kila mwaka Mjini Dar es Salaam.

- Vile vile wanawake waliopata mikopo hiyo na kuitumia vizuri wameweza kusaidia kuboresha nyumba zao na familia zao kwa ujumla.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, katika majibu ambayo yametolewa leo limetolewa jibu zuri sana ambalo linatia moyo kwa wanawake wa Tanzania. Hata hivyo nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa Wizara ya Makamu wa Rais, inayoshughulikia kuondoa umaskini wameshafanya *survey* na inaleta matumaini kwa nchi hii, je, Wizara hiyo inaweza ikaweka dawati katika Wizara ya Jamii, Jinsia na Watoto ili kwa pamoja kwa ujumla wao kwa kutumia *survey* waliyoifanya wakashirikiana kuunda benki ya wanawake nchini ili kusudi badala ya Mifuko kuwa mingi, maana suruali mwisho wake mifuko mitatu, maana mifuko mingi nayo inachanganya watu, kwa hiyo wawe na Mfuko mmoja na ile Mifuko mingine iwe ni wadau wa benki hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, je, kwa kuwa *survey* haijafanyika kwa upande wa wanawake wa Tanzania, je, wanaweza wakawa na *pilot point* ili Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto pamoja na Waziri anayehusika na Kuondoa Umaskini tukafuatana nami kuanza *survey* kwenye Jimbo langu kuanzia Mkulazi, Tegetero kwa gharama za chakula tu kwangu, lakini usafiri kwenu? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa kazungumzia Mifuko, anasema kwenye suruali mifuko ipo mitatu. Lakini mimi naona mifuko ipo mingi tu. Kwa hiyo, kikubwa ni kwamba mifuko ile ijae ina minyang'ure. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa benki, naafikiana na yeye mia kwa mia, lakini naomba tu nitoe taarifa kwamba Wizara imeandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusu uanzishwaji wa Benki ambazo zinakusudiwa kuendeshwa kwa mfumo wa Vyama vya Kuweka na Kukopa yaani *SACCOS.* Kwa hiyo, mchakato huo karibu utakamilika.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa dawati la jinsia, suala la kuondoa umaskini ni tambuka. Kwa hiyo, kama mlivyoona au kusikia, Mawaziri wote waliofika hapa kuwasilisha bajeti zao, bajeti hizo zilikuwa zinalenga katika kuondoa umaskini. Kwa

hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira, tutaingia sasa katika hatua ya pili ya kuondoa umaskini na hayo yote yatazingatiwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Moja ya vigezo ambavyo vinasababisha kuongeza umaskini ni ongezeko la ugonjwa wa UKIMWI hasa Vijijini na kwa kuwa akinamama ndio mara nyingi wamekuwa wakiwahudumia wagonjwa wao kwa kutumia pesa zile zile ndogo ambazo hukopeshwa, je, Wizara sasa itakuwa tayari kuongeza japo hizo pesa za mkopo ziweze kukidhi mahitaji madogo madogo pamoja na kununua dawa za wagonjwa wao? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, mimi najua kabisa *concern* ya Mheshimiwa Venance Mwamoto. Ni kweli kwamba kuna haja ya kuongeza Mifuko hii lakini tatizo ni uwezo, isipokuwa bado naomba niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba agizo la Waziri Mkuu liko pale pale tuwe pamoja katika kuweka asilimia 5 katika Halmashauri zetu kwa ajili ya Mifuko hii ya Wanawake. Kwa upande wa ugawaji wa madawa, ni kweli kama mlisikiliza taarifa ya habari tangu jana hadi leo, kuna mpango maalum wa kugawa dawa za kuongeza muda wa kuishi kwa waathirika wa Ugonjwa wa UKIMWI tayari wameanza kugawa dawa hizo leo hii au jana bure. Ahsante sana. *(Makofi)*

Na. 399

**Ujenzi wa Kituo cha Polisi -Makongolosi**

**MHE. NJELU E. M. KASAKA** aliuliza:-

Kwa kuwa Kituo cha Polisi katika Mji Mdogo wa Makongolosi kinafanya shughuli zake kwenye jengo ambalo halina hadhi na kwa kuwa kutokana na hali hiyo, wananchi wameanza kujenga Kituo kingine chenye hadhi lakini wana shida ya mabati na saruji.

Je, Serikali itawasaidiaje wananchi hao?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mhesimiwa Njelu Kasaka, Mbunge wa Jimbo la Lupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa jengo linalotumiwa kama Kituo cha Polisi katika Mji Mdogo wa Makongolosi halina hadhi. Ni kweli vilevile kuwa wananchi wameanzisha ujenzi wa Kituo chenye hadhi. Kwa msingi huu napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza viongozi na wananchi wa Mji Mdogo wa Makongolosi, pamoja na Mbunge wao Mheshimiwa Njelu Kasaka, kwa moyo wao wa kuanza kutatua tatizo hili kwa njia ya kujitolea. Hii ni hatua sahihi inayopaswa kuigwa na wananchi wa maeneo mengine yanayohitaji Vituo vya Polisi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu iwapo Serikali itatoa msaada, ni kwamba Serikali ina utaratibu wa kuunga mkono nguvu za wananchi pale hali ya fedha inaporuhusu. Kwa hiyo, kama ambavyo tulivyoahidi wakati wa hotuba yetu ya bajeti, Serikali itawaunga mkono wananchi wa Makongolosi ili kuwapa ari ya kukamilisha jengo lao.

Na. 400

**Kituo cha Polisi - Puge**

**MHE. LUCAS L. SELELII** aliuliza:-

Kwa kuwa Kituo cha Polisi Puge kilianzishwa kwa ajili ya kusaidia ulinzi na usalama wa maeneo yaliyo mbali na Mji wa Nzega na kwa kuwa Kituo hicho kinahudumia eneo kubwa sana na kwa kuwa linapotokea tukio lolote la uhalifu, Polisi wa Kituo hicho husafiri kwa baiskeli au miguu kwenda kwenye eneo la tukio; na kwa kuwa, Kituo hicho kipo umbali wa kilometa 60 kutoka Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itakipatia Kituo hicho gari ili kurahisisha usafiri na kuboresha ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucas Selelii, Mbunge wa Jimbo la Nzega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Kituo cha Puge kinahitaji mawasiliano madhubuti kama gari, pikipiki, *radio call* na kadhalika, ili kazi ya kusimamia usalama wa raia na mali zao iweze kufanyika kwa ufanisi.

Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa tatizo la usafiri na mawasiliano kwa ujumla si la Puge pekee, bali linahusu vituo vingine vidogo vya Polisi zaidi ya 600 katika nchi nzima. Serikali inalifahamu tatizo hili ila kutokana na ufinyu wa bajeti, inashindwa kuliondoa kwa mara moja. Kwa kuwa sasa bajeti ya Jeshi la Polisi inaendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka, vivyo hivyo hali ya vitendea kazi itaendelea kuboreshwa mwaka hadi mwaka. Mpango uliopo kwa mwaka huu wa fedha ni kununua magari kwa ajili ya Wakuu wa Polisi wa Wilaya, Vituo vya nje ya Makao Makuu ya Wilaya kama Kituo cha Puge vitaendelea kupata tu huduma ya magari kutoka Makao Makuu ya Wilaya pale inapotokea dharura ya kufanya hivyo.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. La kwanza, kwa kuwa wahalifu au majambazi hufanya uhalifu kwa kutumia magari na vifaa vya kisasa kuliko walivyonavyo Polisi, je, Naibu Waziri anawambiaje askari kama jambazi au mhalifu anapotumia gari, wao watumie baiskeli au waende kwa mguu?

La pili, kwa kuwa vituo hivi vingi alivyovisema viko katika nchi nzima na vilianzishwa vikiwa na bajeti ya kujulikana kwamba viko mbali na Makao Makuu ya Wilaya na kwa kuwa wamefanikisha kuweka magari kwenye Makao Makao Makuu ya Wilaya haoni yale magari yaliyopo sasa kwenye Makao Makuu ya Wilaya yangeenda kwenye Vituo vya Polisi vilivyo mbali kama vile Kituo cha Polisi cha Puge na kingine kiko kule Bukene?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba wahalifu wanavyofanya uhalifu kazi yao wanatumia magari na ili kuwafuatilia ni lazima na Polisi nao wawe na magari. Sasa tatizo linalokuja ni uwezo wa Serikali wa kuvipatia vituo vyote vya Polisi magari. Vituo tu vidogo peke yake viko zaidi ya 600 mbali ya Wilaya. Sasa bajeti waliyotupitishia mwaka huu kwa mfano ni magari 179. Kusema kweli hata kama Mheshimiwa Lucas Selelii na yeye angekuwa hapa nilipo mimi kugawa magari 179 yaenee katika vituo 600 ni jambo ngumu kweli kweli.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba maadam bajeti ya Polisi inaongezeka mwaka hadi mwaka tutaendelea kuongeza magari. Lengo letu kwanza tumalize mahitaji katika Wilaya, tukishamaliza mahitaji ya Wilaya ambapo kila Wilaya itahitaji magari yasiyopungua matatu. Tukishamaliza hapo sasa tutaanza kwenda katika Vituo vya nje. Lakini uwezo uliopo sasa hivi ni kuhudumia magari katika Wilaya na ninaposema Wilaya ni pamoja na Tarafa zake na Kata zake linapotokea tukio mahali radio call tumezisambaza katika vituo vyote watapiga *radio call* gari kutoka Makao Makuu ya Wilaya litakwenda kuhudumia katika eneo husika.

Na. 401

**Kuathirika Kielimu kwa Mtoto wa Kike**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa hivi sasa Serikali yetu imefikia lengo la *MDG's* la kuwapeleka shule watoto wa kike na kiume na kwa kuwa watoto hao hufanya vizuri wawapo katika shule za msingi na uwezo wao huendelea kupungua kadri wanavyoendelea na elimu za juu hasa katika masomo ya sayansi na kwa kuwa Serikali yetu imekuwa ikiridhia itifaki na mikataba mbalimbali ya haki sawa kwa wanawake na wanaume ikiwemo haki ya elimu.

(a) Je, Serikali imeshafanya utafiti wa kina kuona sababu za kimsingi zinazomuathiri mtoto huyo wa kike?

(b) Je, kama utafiti umefanyika ni mikakati gani imeandaliwa ili kuhakikisha tunawasaidia watoto hao wa kike ambao wengine hupata mimba kwa kubakwa au kwa ulaghai?

(c) Je, Serikali haioni kuwa Sheria Na. 25 ya Elimu ya mwaka 1978 inatakiwa ipitiwe upya ili kusaidia kuondoa dhana potofu ya kudhania kwamba kila mtoto apatae mimba shuleni ni malaya?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, lakini kabla ya hapo naomba radhi majibu ni marefu kidogo kwa sababu taarifa zinazotafutwa ni muhimu na zimefafanuliwa kwe kirefu kidogo.

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inazifahamu vizuri sababu zinazomuathiri mtoto wa kike akiwa shuleni na kubaini kama ifuatavyo:-

(i) Watoto wengi kuchelewa kuanza darasa la kwanza na kusababisha wanafunzi wa madarasa ya tano hadi saba katika shule zetu za msingi karibu asilimia 70 kuwa na umri wa miaka zaidi ya 14, ambao ni umri wa Sekondari. Mitaala ya Elimu ya Msingi imeandaliwa kwa ajili ya watoto wa miaka saba hadi 13 wanaoweza kuchanganyika wavulana na wasichana bila matatizo na kufundishwa na kujifunza vizuri. Lakini wakiwa na miaka zaidi ya 14 mabadiliko ya kimaumbile yanawaathiri sana wasichana katika kujifunza na kufundishwa.

(ii) Mila na desturi mbaya zinazoashiria wasichana kuozwa au kuolewa mara wanapopevuka bila kujali kama bado ni wanafunzi.

(iii) Utaratibu mbaya wa mgawanyo wa kazi katika familia ambapo wasichana wanapangiwa kazi nyingi kuliko wavulana.

(iv) Ukosefu wa maadili mema kwa baadhi ya wanaume wanaopenda kuwalaghai wanafunzi wasichana kufanya nao mapenzi.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kumsaidia mtoto wa kike katika kupata haki yake ya elimu, mikakati mbalimbali imeandaliwa na inatekelezwa kama ifuatavyo:-

(i) Imetungwa kanuni iitwayo *The Compulsory Enrolment and Attendance Rules 2002,* inayofanya kutomwandikisha shule mtoto wa miaka saba kuanza darasa la kwanza na kumwachisha shule mtoto wa shule kwa sababu yoyote ile kuwa kosa la Jinai lenye adhabu ya faini na au kifungo kwa anayekiuka.

Kutokana na hatua hii, watoto wa miaka saba wanaoanza darasa la kwanza wameongezeka kutoka asilimia 20.2 mwaka 2000 hadi asilimia 86.3 mwaka 2004. Aidha, watoto wa rika la elimu ya msingi (miaka saba hadi 13) walioko shuleni wameongezeka kutoka asilimia 58.8 mwaka 2000 hadi asilimia 90.5 mwaka 2004.

(ii) Imetungwa kanuni iitwayo *The Education (Imposition of Penalties to Persons who Marry or Impregnate a School girls) Rules 2003,* inayotoa adhabu kali sana ya vifungo na faini kwa anayemuoza, anayemuoa na anayempa mimba mtoto wa shule.

(iii) Serikali imeandaa na inatekeleza MMEM 2004 hadi 2006 na MMES 2004 hadi 2009 inayotoa fursa sawa ya elimu kwa jinsia zote.

(iv) Mada ya Elimu ya Afya na Uzazi imeingizwa katika masomo chukuzi *(Carrier Subjects)* na aidha, imeanzishwa huduma ya malezi na ushauri nasaha katika shule na Vyuo.

(c) Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Sheria ya Elimu na 25 ya mwaka 1978 haina dhana potofu ya kudhania kila mtoto apataye mimba shuleni ni malaya. Sheria hiyo imemtaka Waziri atunge kanuni inyotaja makosa yatakayo sababisha mtoto wa shule afukuzwe.

Katika kutekeleza matakwa ya sheria hiyo, Waziri ametunga kanuni *iitwayo The Education (Expulsion and Exclusion of Pupils from schools) Regulations,2002,* katika kanuni hiyo Waziri ameyataja makosa ya aina tatu yatakayosababisha mwanafunzi afukuzwe shule ambayo ni kama ifuatavyo:-

(i) Ukiukaji wa maadili mema na utovu wa nidhamu kwa ujumla yanayoharibu jina la shule.

(ii) Kupatikana na makosa ya jinai kama vile wizi, uharibifu wa mali,umalaya, utumiaji wa madawa ya kulevya na matendo ambayo ni kinyume cha maadili.

(iii) Mwanafunzi kujiingiza katika ndoa.

Mwanafunzi anapofukuzwa shule kwa kosa la mimba huwa ni kwa kipengele cha kwanza yaani cha ukiukaji wa maadili mema ya jamii na siyo kwa kosa la umalaya kwa sababu kupata mimba si lazima kutokane na umalaya. Mwanafunzi anaweza kufukuzwa shule kwa kosa la umalaya bila kuwepo tukio la mimba. Makosa yote hayo yanaweza kumfukuzisha mwanafunzi shule, msichana au mvulana, bila ubaguzi. Mwanafunzi mvulana anaweza kufukuzwa shule kwa kosa la kumpa mimba mwanafunzi msichana au mwanamke mwingine yeyote.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa ruhusa ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa baada ya Wizara kugundua tatizo hilo la watoto wa kike ambao wamekumbana na matatizo mengi mbalimbali kutokuweza kumaliza Elimu ya Msingi walianzisha Mpango wa MEMKWA ili kuhakikisha watoto hao wote wanaendelea na masomo ya Elimu ya Msingi, je, Wizara haioni kwamba ni wakati muafaka sasa kuanzisha mpango kama huo katika Elimu ya Sekondari ili kuwaokoa watoto hao ambao

wamepata matatizo ya namna moja ama nyingine na kuwasababishia kutokupata Elimu ya Sekondari katika muda unaotakiwa? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI):** Mheshimiwa Spika, napenda kuamini kwamba wazo lake la utaratibu wa MEMKWA kwa maana ya Elimu kwa wale waliokosa Elimu ya Msingi nje ya umri tulioutaja katika majibu ya msingi huangaliwe katika Elimu ya Sekondari, wazo lake tutalifanyia kazi na tutaona kama linatekelezeka.

Na. 402

**Majengo Chakavu - Chuo cha Elimu Kitangari**

**MHE. LYDIA T. BOMA** aliuliza:-

Kwa kuwa majengo ya Chuo cha Elimu Kitangari yakiwemo mabweni, madarasa, ofisi, nyumba za wakufunzi na wafanyakazi ni chakavu mno hali ambayo inatishia usalama wa wanafunzi, wakufunzi na wafanyakazi wote kwa ujumla Chuoni hapo:-

(a) Je, Serikali inayo taarifa na matatizo haya yanayokikabili Chuo hicho?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani za haraka iwezekanavyo za kunusuru mali, familia za wakufunzi na Wanachuo kutokana na hali hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lydia Thecla Boma, Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Chuo cha Ualimu cha Kitangari kilichoko Wilaya ya Newala, Mkoa wa Mtwara kina jumla ya wanafunzi 205, wakufunzi 11, watumishi wengine 14 na walimu wa shule ya mazoezi 8. Serikali inafahamu matatizo yanayokikabili Chuo hicho, hususan ya uchakavu na upungufu wa majengo kama ilivyo katika baadhi ya shule za Sekondari na Vyuo vingine vya Ualimu.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) ilitenga na kutoa fedha za kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia ya Vyuo vya Ualimu kwa lengo la kuboresha Elimu ya Ualimu. Tatizo la uchakavu wa majengo na samani katika Chuo cha Ualimu Kitangari linaendelea kutatuliwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2002/2003 Serikali ilitoa kiasi cha shilingi 13,270,768/= na katika mwaka 2003/2004 Serikali ilitoa kiasi cha shilingi 7,500,000/= kwa ajili ya ukarabati

mdogo na kuongeza samani katika Chuo cha Ualimu Kitangari. Kwa hiyo jumla kwa miaka miwili mfululizo zimetolewa shilingi 20,770,768/= kwa ajili ya ukarabati wa Chuo cha Elimu cha Kitangari.

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kabla sijauliza maswali hayo, niishukuru Serikali kwa jinsi ilivyoweza kutatua matatizo mbalimbali ambayo yalikuwa ni kero katika Chuo cha Ualimu Kitangari.

La kwanza, hiki Chuo kiko umbali wa maili 25 kufika Makao Makuu ya Wilaya na hawana mawasiliano ya kiurahisi kama simu na usafiri wa uhakika, je, Wizara inakisaidiaje hiki Chuo kwa sababu ni suala muhimu sana kupata simu?

La pili, kwa kuwa Wanachuo Walimu hupata tabu jinsi ya kupata mikopo ya kuweza kuwasaidia kununua mahitaji mbalimbali wakati wanapokwenda Chuoni, je, kutokana na bajeti ya Wizara mwaka huu jinsi ya kuwasaidia Walimu nchini ikiwemo na Kitangari itawasaidiaje?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI):** Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mawasiliano ya simu pale Chuoni kwa sababu kiko maili 25 kutoka Makao ya Wilaya.

Ningependa niseme tulipata Semina hapa wakati wa Mkutano huu wa Bunge kutoka Kampuni ya Simu Tanzania kwa kutueleza mipango ambayo wanayo kueneza simu karibu sehemu zote nchini. Ninaamini Chuo hiki hakitasahaulika kwa sababu ni sehemu ambayo Kampuni ya Simu Tanzania itapata wateja na kwa maana hiyo kupata mapato yake.

Mheshimiwa Spika, la pili kuhusu Wanachuo Walimu kupewa mikopo na kwamba katika bajeti ya Wizara hii itaangaliwa namna gani ili wasaidiwe. Kama tumetoa sehemu ambayo ni kuwezesha Walimu kupata mikopo na kama ni utaratibu hata unaohusu Walimu wanafunzi wa Ualimu bila shaka hawatabaguliwa katika suala hili.

Na. 403

**Umeme Vijijini Kondoa**

**MHE. PASCHAL C. DEGERA** aliuliza:-

Kwa kuwa vijiji vya Dalai, Pongai, Waida, Piho, Jenjeluse Igunga, Mapango, Madaha, Isasumya, Nkulari na Songambele vipo karibu sana na njia ya umeme inayotoka Mjini Kondoa kwenda Kibaya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuvipatia umeme vijiji hivyo?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paschal Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, kama ifuatavyo:-

Baadhi ya vijiji vilivyotajwa na Mheshimiwa Mbunge vimepitiwa na njia ya umeme inayotoka Kondoa kwenda Kibaya. Kijiji cha Jenjeluse kimepangwa kupatiwa umeme mwaka huu. Vijiji vya Piho, Igunga, Madaha, Isasumya, Nkulari na Songambele viko karibu na kijiji cha Soya ambacho kimepangwa kupatiwa umeme chini ya Mpango wa *Electricity IV* awamu ya pili. Kijiji cha Soya kikishapatiwa umeme chini ya Mapngo huo ndipo vijiji nilivyovitaja vitaunganishwa kutokea hapo Soya. Kijiji cha Soya kinategemea kupatiwa umeme mwaka 2005 kwa gharama ya shilingi milioni 105.

Mheshimiwa Spika, vijiji vingine vilivyosalia vitapatiwa umeme kulingana na upatikanaji wa fedha. Makisio ya gharama za utekelezaji ni kama ifuatavyo:-

| Kijiji | Umbali kutoka njia ya umeme ya Kondoa - Kibaya | Gharama |
|---|---|---|
| Dalai | 7 km | 90 milioni |
| Pongai | 8 km | 104 milioni |
| Mapango | 2.5 km | 32.5 milioni |
| Jumla | 17.5 km | 226.50 milioni |

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa bajeti ya Serikali, vijiji hivyo na vingine nchini vitaendelea kupatiwa umeme kulingana na upatikanaji wa fedha Serikalini.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

La kwanza, kwa kuwa Serikali ilikwishaahidi kwamba vijiji vya Hamai na Soya vingepatiwa umeme mwaka huu, je, ni sababu ipi ambayo imefanya Mheshimiwa Waziri atamke leo kwamba vijiji hivyo vitapatiwa umeme mwaka kesho?

La pili, kwa kuwa vijiji nilivyovitaja katika swali la msingi viliahidiwa na Serikali kupatiwa umeme katika awamu ya pili ya *Electricity IV* sasa ni tatizo gani ambalo linafanya Mheshimiwa Waziri asite kukubali vijiji hivi vipatiwe umeme katika awamu hii ya *Electricity IV?*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwanza ilikuwa ni kwa nini vijiji vya Hamai na Soya havipatiwi umeme mwaka huu?

Mheshimiwa Spika, tatizo la kutotimiza ahadi hiyo au azma hiyo ni kwamba Shirika la *TANESCO* hasa tangu mwaka jana mpaka sasa hivi limekuwa na tatizo la uhaba wa mapato yaliyotokana na ukame ambao uliigharimu *TANESCO* fedha nyingi sana kuzalisha umeme ili Taifa lisije likaingia kwenye mgao. Kwa hiyo, ililazimika *TANESCO* iahirishe miradi yake mingine ya kupeleka umeme mahali ambapo ahadi ilikuwa imetolewa. Lakini azma iko pale pale na vijiji hivi kama nilivyosema vitapatiwa umeme kwa wakati huo ambao nimeutaja hapo.

Mheshimiwa Spika, vilevile awamu ya pili ya vijiji vya *Electricity IV* ambavyo Mheshimiwa Mbunge amevitaja navyo tatizo ni hilo hilo la kwamba tumeahirisha ilibidi tu *postpone* au to *push forward* utekelezaji wa miradi mingi sana ambayo tulikuwa tumefikiria tutaitekeleza mapema kwa sababu hiyo ya matatizo ya fedha katika Shirika hilo. Lakini namwaahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba ahadi iko pale pale na wananchi wa vijiji hivyo wavute subira watapatiwa umeme mara tu fedha zitakapopatikana na utekelezaji utaanza.

Na. 404

**Migodi Iliyokuwa Imemilikiwa na Serikali**

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED** aliuliza:-

Kwa kuwa kabla ya kubinafsisha na kukaribisha wawekezaji kwenye madini Serikali ilikuwa na migodi yake;-

(a) Je, ni migodi ya aina gani ilikuwepo?

(b) Je, ni migodi mingapi na ya aina gani ambayo Serikali ilikuwa imemiliki au kuwa na hisa?

(c) Je, Serikali imepata mapato kiasi gani kutokana na hisa zake kwenye migodi hiyo?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Kuteuliwa, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Migodi iliyokuwepo ilikuwa na dhahabu, almasi, madini ya mbolea *(Phosphate),* chumvi, makaa ya mawe, udongo mweupe wa *Kaolin,* vito na madini ya kutengeneza vito *(meerschaum).*

(b) Kupitia Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO),* Serikali ilikuwa inamiliki hisa asilimia 100 kwa 100 katika migodi yote isipokuwa katika mgodi wa almasi wa *Williamson Diamonds Limited* ambapo Serikali ilikuwa na hisa asilimia 50.

Mheshimiwa Spika, katika Kampuni ya *Nyanza Salt Mines Tanganyika Limited,* Serikali ilikuwa na hisa asilimia 81 na migodi wa *Mundarara Ruby Mining,* Wilayani Monduli, Serikali ina hisa asilimia 50. Migodi mingine ilikuwa ifuatayo:-

Mgodi wa *Buckreef Gold Mining Limited,* Geita ambao Serikali imeingia Mkataba na Kampuni ya *East Africa Mines Limited* kutoka Australia kufanya upenguzi yakinifu wa mashapo ambapo hisa za Serikali katika mgodi huo zitakuwa asilimia 20 kama uzalishaji utaanza tena. Mgodi wa *Lupa Gold Mining Limited,* Wilayani Chunya ambao ulifilisika, Mgodi wa *Tanganyika Meerschaum Corporation Limited* uliokuwa katika eneo la Sinya Magharibi mwa Mlima Kilimanjaro ambao ulijaa maji na kufungwa, Mgodi wa *Minjingu Phosphate Company Limited,* Mgodi wa *Pugu Kaolin Limited,* Wilayani Kisarawe, Mgodi wa Makaa ya Mawe wa *Kiwira Coal Mines Limited,* Kampuni ya *Coastal Saltworks Limited* ilikuwa na mashamba ya kuvuna chumvi Saadani, Changwahela na Kitame na Uvinza Kigoma .

(c) Kupitia Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma *(PSRC)* Serikali imeuza hisa zake zote katika Kampuni za *Coastal Saltwork Limited* na *Nyanza Salt Mines Tanganyika Limited* na nusu ya hisa zake katika mgodi wa *Williamson Diamonds Limited.* Mauzo yalikuwa jumla ya *US$705,303* na shilingi za Kitanzania 556,833,129/= kwa mchanganuo ufuatao:-

*Coastal Saltworks Limited US$524,761, Nyanza Salt Mines Limited shilingi* 500,152,012/=, *Pugu Kaolin Mine* shilingi 56,681,117/= na *Williamson Diamonds Limited US$ 180,542.*

Aidha, kupitia Mfuko wa Udhamini wa Mikopo na Madeni *(The Loans and Advances Realization Trust - LART),* mwaka 2001, Serikali iliuza Kampuni ya *Minjingu Phosphate Company Limited* kwa Kampuni ya *Fibre Board* ya Arusha kwa shilingi milioni 720. Mwaka 1999, Serikali pia iliuza hisa asilimia 5 kwa *US$* milioni tano ambazo ilitakiwa ipate katika mgodi wa Bulyanhulu kwa mujibu wa mkataba kati ya Serikali na Kampuni ya *Kahama Mining Corporation Limited.* Hisa hizo ziliuzwa kabla ya mgodi kujengwa.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba kuuliza maswali ya nyongeza.

La kwanza, kwa kuwa sheria zote za nchi zinatokana na Katiba ya Nchi na kwa kuwa unapovunja Sheria ya Nchi maana yake umevunja Katiba ya Nchi na kwa kuwa *Procurement Act* inataka biashara yoyote inayofanywa na Serikali iwe wazi; na kwa kuwa hisa hizi zimeuzwa za *Williamson Diamonds Limited* haikutangazwa kwenye *tender,* haikuwa wazi. Je, Serikali inakubali kwamba imevunja Katiba ya Nchi kwa kuvunja Sheria hiyo?

La pili, kwa kuwa hisa zilizouzwa *Williamson Diomands Limited* ni asilimia 25 kwa dola za Kimarekani 180,542 kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, je, haioni kwa

kufanya hivyo imeikosesha mapato Serikali kwa makusudi na wanaohusika wanahitaji kuchukuliwa hatua? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, Serikali inafuata Katiba na sheria ambazo zipo na katika mikataba yote ambayo Serikali inatiliana saini na mnunuzi au muuzaji tunakuwa makini sana kuhakikisha kwamba hatuvunji Katiba wala Sheria na tuna Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa kutushauri katika jambo hilo na mikataba ambayo imeundwa kisheria tunaifuata kifungu kwa kifungu.

Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed , kwamba hatukuvunja Katiba wala sheria yoyote na kama ana ushahidi wa namna hiyo basi anaweza kuuleta akatuonyesha ni wapi tumevunja ili tusifanye hivyo tena.

Vilevile katika kuuza hisa za *Williamson Diamonds Limited,* hatujavunja yaani tusije tukafanya hivyo, alete ushahidi wowote unaoonyesha pale tulipovunja, lakini tunaamini sisi kama Serikali hatujavunja sheria wala Katiba ya nchi.

Mheshimiwa Spika kuhusu uuzaji wa *shares* za *Williamson Diamonds* vile vile tulifuata mikataba, sheria na taratibu zilizokuwepo na hatukuvunja taratibu yoyote. Kama Mheshimiwa Mbunge anataka maelezo zaidi anaweza kuja kutuona tutamwelekeza vizuri. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, napenda tu niongozee kwa majibu yake mazuri kwa kusema ifuatavyo kuhusiana kwa nini hisa za *Williamson Diamonds* hazikutangazwa kama alivyouliza Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, *Williamson Diamonds* ni Kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni hapa nchini. Kwa mujibu wa makubaliano ambayo misingi yake inatokana na Sheria hiyo ya Kampuni mhisa au wanahisa wakiamua kuuza hisa au mmoja wao akiamua kuuza hisa sheria inamtaka ampe kwanza haki yake mhisa huyo. Iwapo mhisa huyo atashindwa kumudu bei ambayo anataka ziuzwe hisa hizo basi mwenye hisa ambaye anataka kuuza ndiyo anaruhusiwa sasa kuziuza hisa zake nje ya wanahisa hao. Huo ndio utaratibu wa Makampuni unaotumika sio Tanzania peke yake lakini unatumika katika nchi nyingi tu.

**SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha na maswali yote ya nyongeza yamejibiwa. Sasa matangazo.

Kwanza leo jioni baada ya kufunga Mkutano huu wa Bunge wa Kumi na Sita, kama kawaida yake Mheshimiwa Waziri Mkuu ameandaa tafrija ya kuagana. Kadi za mwaliko ziko kwenye *pigeon hole* lakini tujue tu kwamba sisi sote tumealikwa kuhudhuria tafrija hiyo mara baada ya kumaliza shughuli za hapa moja kwa moja tunakwenda kwenye viwanja vyetu vya burudani.

Pili, ni taarifa ya vikao vya Kamati za Kudumu. Wanaojua vizuri kalenda za mwezi Mtukufu wa Ramadhani wameniambia kwamba hizi kalenda za Serikali

wamekosea, haiwezekani *Idd El Fitri* iwe Oktoba. Lakini ndivyo kalenda zinavyoonyesha. Kwa hiyo, tunaomba kusahihisha basi kwamba badala ya vikao kuanza tarehe 20 Oktoba, 2004 ambayo ni Jumatano sasa vikao vitaanza siku ya Jumatatu tarehe 18 Oktoba, 2004 ili tupate wiki mbili kamili za vikao vya Kamati. Naomba kufanya masahihisho hayo kwenye taarifa ya kalenda za vikao.

Matangazo ya vikao vya Kamati, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* anatangaza kikao cha Kamati hiyo leo tarehe 6 Agosti, 2004 kuanzia saa 6.00 mchana kwenye chumba namba 219 na Kamati ya Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa Anne Makinda, anawatangazia Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba kuna kikao leo saa 5.00 asubuhi chumba namba 231, ghorofa ya pili. Hizo ni Kamati za Kudumu.

Vikao vingine visivyokuwa vya Kamati za Bunge ni *TAPAC.* Wanachama wote wa *TAPAC* wanaarifiwa na Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mwenyekiti wao kwamba kutakuwa na kikao saa 7.00 mchana chumba namba 231.

Halafu kuna *APNAC* ya Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mwenyekiti, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Utendaji sio wote, ni Kamati ya Utendaji wa *APNAC* kwamba kutakuwa na kikao saa 7.00 mchana chumba namba 428 ghorofa ya nne. Mwisho wa matangazo. Ngoja tuone kama kuna lingine. Hapana mwisho wa matangazo, Katibu endelea na *Order Paper.*

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira wa Mwaka 2004**
***(The Environmental Management Bill, 2004)***

**Muswada wa Sheria ya Utaratibu wa Kuwaenzi Waasisi wa Taifa wa Mwaka 2004 *(The Founders of the Nation (Honouring Procedures) Bill, 2004)***

**Muswada wa Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2004**
***(The Public Procurement Bill, 2004)***
**Muswada wa Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji wa Kiuchumi wa Mwaka 2004 *(The National Economic Empowerment Bill, 2004}***

*(Miswada iliyotajwa hapo juu ilisomwa Bungeni Mara ya Kwanza)*

## HOJA ZA SERIKALI

## AZIMIO

### Azimio la Kumwezesha Waziri wa Fedha Kufuta au Kusamehe Madai au Hasara Itokanayo na Upotevu wa Fedha au Vifaa vya Serikali

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Azimio la Kumwezesha Waziri wa Fedha Kufuta au Kusamehe Madai au Hasara ambazo hazilipiki zitokanazo na Upotevu wa Fedha na Vifaa vya Serikali kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni, 2003 kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Mwaka 2001. Aidha, Azimio lilipata ridhaa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali *(PAC)* katika kikao chake cha tarehe 28 Julai, 2004 kilichofanyika hapa Mjini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali *(PAC)* Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Kuteuliwa pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa maoni yao mazuri yenye lengo la kuboresha udhibiti na uimarishaji wa usimamizi wa mali za vifaa vya Serikali kwa lengo la kupunguza au kuepuka upotevu wa mali na vifaa hivyo.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba katika Bunge la Bajeti la mwaka wa fedha 2003/2004 Bunge lako Tukufu lilipitisha Azimio la Kufuta au Kusamahe Madai ya Hasara ambazo hazilipiki zitokanazo na upotevu wa fedha au vifaa vya Serikali ya kiasi cha shilingi 72,850,017,122.30 kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni 2002.

Aidha, wakati wa kuwasilisha Azimio hilo Mheshimiwa Waziri wa Fedha alitoa maelezo kwamba bado Serikali ina potevu nyingine ambazo zinafanyiwa kazi na mara baada ya kuanza kukamilika na kujadiliwa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali, Serikali itawasilisha hoja Bungeni kuomba kufuta au kusamehe potevu hizo.

Mheshimiwa Spika, Azimio ninalowasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu linakusudia kufuta na kusamehe madeni, hasara na potevu ambazo hazilipiki katika kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni, 2003.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa ambayo naiwasilisha mbele ya Bunge hili hasara husika zimegawanyika katika sehemu kuu tatu. Mgawanyo huu umelenga kuainisha kwa uwazi zaidi hasara hizo ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuzielewa vizuri na hatimaye kufikia uamuzi ulio sahihi. Hasara hizo ni kama ifuatavyo:-

(a) Zile zinazohusu potevu za fedha na vifaa shilingi 1,322,313,374.39.

(b) Zile zinazohusu mapato au maduhuli yaliyoshindikana kukusanywa ya shilingi 46,334,898,346.69.

(c) Zile ambazo zinahusu usawizishaji wa kumbukumbu katika vitabu shilingi 164,280,398.95.

Mheshimiwa Spika, jumla yote ni shilingi 47,821,492,120.03. Maelezo ya hasara hizo ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, hasara zinazohusu potevu za fedha na vifaa za shilingi 1,322,313,374.39 zimetokana na sababu mbalimbali zikiwemo wizi wa mali ikiwa ni pamoja na fedha, kushuka kwa thamani ya shilingi kulinganisha na fedha za nje yaani *exchange rates loses,* ubadhirifu, kusinyaa kwa bidhaa kama vile chakula yaani *shrinkage,* vifaa kupitwa na wakati muhukizo *(evaporation)* kama vile mafuta uzembe na pia kwa ajili ya uzembe yaani *negligency.*

Pili, hasara zingine zinazoombewa kufutwa ni zile za shilingi 46,334,898,346.69 ambazo zinatokana na mapato yaliyoshindikana kukusanywa. Makusanyo yaliyoshindikana ni pamoja na shilingi 14,570,730,146.09 ambazo ni hasara inayotokana na kodi na mapato mengine mbalimbali ambayo Serikali ilikuwa inadai Mashirika ya Umma yaliyobinafsishwa au kufilisiwa.

Aidha, kwa kuwa wawekezaji wanaonunua Mashirika yaliyobinafsishwa hawataki kurithi Madeni ya Mashirika wanayoyanunua Serikali inalazimika kufuta madeni yake kutoka kwa Mashirika hayo.

Aidha, yale madeni ya Mashirika ambayo Serikali ilikopa au kuthamini kutoka nje kama vile Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika na kadhalika au wote wakopeshaji Serikali inawasemehe Mashirika hayo lakini inawajibika kwa kuwalipa kwa wakopeshaji hao wa nje.

Tatu, ni hasara zinazotokana na usawazishaji wa kumbukumbu wa vitabu zinazotufikia shilingi 164,280,398.95. Hasara hizi zinatokana na tatizo la kutofuata taratibu kikamilifu na madai kati ya Idara kwa Idara za Serikali.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikisha Bunge lako Tukufu kwamba Serikali inaweka juhudi katika kusimamia kikamilifu Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 kwa lengo la kupunguza na hatimaye kuepuka hasara za namna hii. Juhudi hizo ni pamoja na kutoa elimu kwa watendaji, kuwaajiri Wahasibu wenye uwezo wa kuhasibu, kuimarisha teknolojia ya usimamizi wa fedha za umma na kanuni za utendaji Serikalini.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaomba kufuta hasara na kusamehe madai ambayo hayalipiki vifaa vya Serikali vya kiasi cha shilingi 47,821,492,120.03 kama ilivyoainishwa katika jedwali ambalo limeambatanishwa pamoja na Azimio hili ambalo limetolewa Waheshimiwa Wabunge ili kutoa picha halisi ya hali ya fedha na mali pamoja na kuondoa Hoja za Ukaguzi kwa Idara na Wizara mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba sasa kuwasilisha Azimio la Bunge la Kufuta na Kusamehe Madai na Hasara Itokanayo na Upotevu wa Fedha na Vifaa vya Serikali kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni, 2003 kama ifuatavyo:-

KWA KUWA kwa mujibu wa Kifungu cha 5 cha Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Fedha za Umma ya mwaka 2001, Waziri wa Fedha anayo mamlaka ya kusimamia na kudhibiti matumizi ya fedha za umma na kutoa taarifa Bungeni;

NA KWA KUWA kwa mujibu wa Kifungu cha 43(1) cha Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Fedha za Umma ya Mwaka 2001, Bunge linaweza, kwa Azimio, kutoa idhini kwa Waziri wa Fedha kufuta hasara itokanayo na upotevu wa fedha, vifaa vya Serikali, madai ya kodi pamoja na riba itokanayo na malimbikizo ya kodi;

NA KWA KUWA vitabu vya Hesabu za Serikali vimeonyesha upotevu wa fedha za Serikali pamoja na maduhuli yaliyoshindikana kukusanywa;

NA KWA KUWA kutokana na upotevu na upungufu huo wa fedha, vifaa na maduhuli ya Serikali upo umuhimu wa kusawazisha kumbukumbu katika vitabu vya Serikali;

KWA HIYO BASI, kwa mujibu wa Kifungu cha 43(1) cha Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Fedha za Umma ya mwaka 2001, sasa Bunge hili linaazimia kumuidhinisha Waziri wa Fedha asamehe na kufuta upotevu wa fedha, vifaa na makusanyo ya maduhuli ya Serikali na kwa ajili hiyo, kusawazisha kumbukumbu katika vitabu vya Serikali kama ifuatavyo:-

(a) Upotevu wa fedha na vifaa shilingi 1,322,313,374.39;

(b) Mapato au maduhuli yaliyoshindikana kukusanywa shilingi 46,334,898,346.69; na

(c) Usawazishaji wa kumbukumbu katika vitabu shilingi 164,280,398.95. Jumla kuu ni shilingi 47,821,492,120.03.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya potevu hizi yapo kwenye kabrasha ambalo naamini Waheshimiwa Wabunge wamepata nakala yake.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA (k.n.y. MHE. HAMAD RASHID MOHAMED - MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali, naomba niwasilishe Taarifa ya Kamati Kuhusu Upotevu wa Fedha na Vifaa vya Serikali katika kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni, 2003.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Rungwe na kwa niaba ya Kamati, kwa masikitiko makubwa naomba nitumie nafasi hii ya awali kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa mjane, familia na wananchi wa jimbo la Uchaguzi la Mbeya Vijijini kufuatia kifo cha aliyekuwa Mbunge wao Marehemu Mheshimiwa Yete Sintemule Mwalyego. Aidha, natoa rambirambi nyingine kwa mjane, familia na wananchi wa Jimbo la Ulanga Mashariki, kufuatia kifo cha aliyekuwa Mbunge wao ndugu yetu mpendwa Marehemu Mheshimiwa *Comrade* Capt. Theodos Kasapira, Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu hawa mahali pema peponi na awape ndugu na jamaa wa Marehemu pamoja na wapigakura wao moyo wa subira.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ya Hesabu za Serikali na kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, kifungu Na. 43(5) na kifungu kidogo cha (b) Toleo la 2004 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati ya Hesabu za Serikali juu ya Azimio la Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuhusu kufuta upotevu wa fedha na vifaa vya Serikali.

Kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mama Blandina Nyoni, Mhasibu Mkuu wa Serikali, kwa jinsi alivyowasilisha kwenye Kamati maelezo ya kina na yenye ufafanuzi kuhusu madhumuni ya Azimio hili. *(Makofi)*

Aidha, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, Waziri wa Fedha na Manaibu Mawaziri wake Mheshimiwa Dr. Festus Limbu na Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatibu, kwa kazi nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

Vile vile napenda kumshukuru Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatibu, Naibu Waziri, ambaye alijumuika na Kamati katika kupitia na kuchambua taarifa ya upotevu tangu ilipowasilishwa kwenye Kamati hadi mwisho. Ahsante sana Mheshimiwa Abdisalaam. Mchango wake na ufafanuzi alioutoa kwenye Kamati ulisaidia kwa kiwango kikubwa kurahisisha kazi ya Kamati.

Aidha, napenda kuwapongeza wafanyakazi wote wa Wizara ya Fedha wakiongozwa na Makatibu Wakuu Grey Mgonja na Ndugu Peniel Lyimo, kwa namna wanavyosimamia vizuri Wizara hii. Sisi sote ni mashahidi kwamba Wizara ya Fedha imejitahidi kuboresha mambo mengi katika kipindi kifupi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mkosefu wa fadhila kama sitawashukuru Waheshimiwa Wabunge wa Kamati yangu kwa ushirikiano wanaouonyesha katika utendaji wa shughuli za Kamati. Nawashukuru Wajumbe wa Kamati kwa kutanguliza maslahi ya Taifa mbele na kuacha tofauti za kisiasa. Ni kwa njia hii tu Bunge linaweza

kusimamia mapato na matumizi ya Serikali kwa lengo la kuwa na Serikali inaowajibika kwa umma wa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niwatambue Wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mwenyekiti, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Emmanuel Kipole, Mheshimiwa Remidius Kissassi, Mheshimiwa Abdul Lutavi, Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, Mheshimiwa Monica Mbega, Mheshimiwa Aridi Uledi, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Leonard Shango, Mheshimiwa Asha Ngede na mimi mwenyewe Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa. Pia tunamshukuru Katibu wetu, Ndugu Anselm Mrema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha chimbuko la Azimio hili ni sheria mpya ya fedha iliyopitishwa na Bunge hili pamoja na kanuni zake. Maafisa Wahasibu wana jukumu la kuhakikisha kwa Mapato na Matumizi ya Serikali yanakusanya na kutumiwa kama ilivyokusudiwa na ilivyoidhinishwa na Bunge na kuhakikisha kwamba hasara hazitokei.

Mheshimiwa Spika, lakini kutokana na sababu mbalimbali hasara hutokea kwa mfano kutokana na wizi, upotevu wa vifaa na vile vile kushindwa kukusanya Mapato ya Serikali. Kabla ya Sheria hii mpya kupitishwa Waziri wa Fedha alikuwa na mamlaka ya kisheria ya kufuta madeni hayo. Lakini baada ya sheria mpya kupitishwa mwaka 2001 mamlaka hayo yakahamishwa na Bunge la Jamhuri la Muungano la Tanzania ndilo lenye jukumu hilo.

Sheria inatamka wazi kuwa taarifa ya hasara na potevu za Serikali ziandaliwe na Mhasibu Mkuu wa Serikali na kuwasilishwa mbele ya Kamati ya Hesabu za Serikali ambayo itachunguza na hatimaye kutoa mapendekezo ya ama kufuta madeni hayo au kupendekeza hatua nyingine kuchukuliwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika,ni kutokana na utaratibu uliotajwa hapo juu Kamati ilikutana kwa idhini yako tarehe 27 na 28 Julai, 2004 na kufanya kazi hiyo. Nataka kuchukua fursa hii kumpongeza Ndugu Francis Mhilu kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuchukua nafasi ya Naibu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Ndugu Mhilu alishiriki kikamilifu katika zoezi zima la kuchambua na kuzifanyia kazi hasara hizo pamoja na kwamba yeye ni mgeni katika ofisi hiyo. Taarifa ninayoiwasilisha hapa mbele ni matunda ya juhudi za pamoja za Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali na Kamati yake.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa hasara na potevu za vifaa vya Serikali zenye jumla ya shilingi 50,763,869,040.03 kama ifuatavyo:-

Hasara zinazohusu potevu za fedha na vifaa shilingi 1,322,313,374.39.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliridhika kwa kiasi cha shilingi 1,322,313,374.39 kinachohusu potevu za fedha na vifaa kifutwe ikizingatiwa kwa hasara inayohusika ya

miaka mingi iliyopita kuanzia ya miaka ya 1980. Chache ni kati ya miaka 1990 hadi kufikia mwezi Juni, 2003.

Aidha, kiasi kikubwa cha hasara kimetokana na sababu mbalimbali zikiwemo za wizi, kushuka kwa thamani ya shilingi yetu katika masoko ya dunia, ubadhirifu, kusinyaa kwa mali, kupitwa na wakati, uzembe na malipo batili ambayo yalifanyika bila Serikali kunufaika na huduma yoyote.

Kamati inawasisitizia Maafisa Wahasibu kuzingatia taratibu, kanuni na sheria za fedha wakati wa kuidhinisha malipo. Hii itasaidia kuondokana na baadhi ya sababu zinazochangia kusababisha hasara hizo na namba mbili ni mapato na maduhuli yaliyoshindikana kukusanywa shilingi 46,334,898,346.69.

Mheshimiwa Spika kasoro hizi zinatokana na Serikali kushindwa kukusanya kiasi hicho cha fedha. Maduhuli haya yalishindikana kukusanywa kutokana na sababu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano mabadiliko ya Sheria za Ukusanyaji, matokeo ya ubinafsishaji, gharama za ukusanyaji kuwa kubwa kuliko kiasi kilichopatikana, maamuzi mbalimbali ya Mahakama kufilisika kwa baadhi ya Mashirika ya Umma chini ya *PSRC* na *LART* na baadhi ya wadaiwa kutojulikana waliko baada ya kuhamisha au kufunga biashara zao.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa katika Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, Viwanja vya Ndege vya Kimataifa vya Dar es Salaam na Kilimanjaro vimekuwa vikidai maduhuli mengi kwa wapangaji wa vyumba vya maduka na Ofisi za Mawakala wa Ndege.

Aidha, Mashirika na Makampuni mengi ya Ndege yamekuwa yakidaiwa ushuru wa kutua na kuegesha. Lakini maduhuli hayo yameshindikana kukusanywa kutokana na baadhi ya Mashirika hayo kufunga biashara zao. Kwa mfano, *Air Zaire, Angola Airline, Air Botswana, Air Burundi, Aeroflot Airline* na kadhalika ambao zamani walikuwa na biashara katika viwanja vyetu lakini sasa hivi hizi ndege hazitui katika hivyo viwanja. Aidha, Shirika la Ndege la Tanzania ilibinafsishwa kubadili jina na imekuwa vigumu kisheria kulidai kwa kuwa halipo tena.

Vile vile Kamati imebaini kuwa kuna madeni ya Serikali kwenye Mashirika ya Umma ambayo baada ya kubinafsishwa madeni hayo yamepelekwa Serikalini. Hivyo basi kwa kuwa Serikali ndiyo mwenye hayo Mashirika haiwezekani kwamba Serikali ikaidai Serikali hiyo hiyo.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha tatu, ni biashara zinazohusu urekebishaji wa kumbukumbu na kiasi kinachohojiwa hapa ni shilingi 164,280,398.95/=.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa hasara hizi zinatokana na kukiuka taratibu, kanuni na sheria za fedha mathalani baadhi ya Mikoa na Ofisi zetu za Ubalozi

zimekuwa zikikopesha masurufu na karadha bila ya kuzingatia taratibu, kanuni na sheria za kwa baadhi ya Maafisa wanapotembelea kikazi maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, katika haya makundi matatu ambayo jumla kuu ni takribani shilingi 47,821,492,120.03.

Kundi la maduhuli na mapato ambayo yalishindikana kukusanya ndiyo kubwa na linachukua asilimia 96.9. Ningependa vilevile niseme kwamba, kuna potevu ambazo zinaendelea kufanyiwa kazi shilingi 2,942,376,920/=

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipatiwa taarifa ya hasara ambazo zimeripotiwa na Wizara, Idara na Mikoa, kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2001. Kamati imeagiza hasara hizi zifanyiwe kazi na ziwasilishwe kwenye Kamati hapo zitakapokuwa tayari. Kamati imependekeza yafuatayo:-

(i) Mheshimiwa Spika, Kamati inabaini kuwa upotevu wa vifaa haupewi umuhimu mzito kama vile upotevu wa fedha. Hivyo, Kamati inasisitiza Serikali itoe umuhimu kwa potevu ya vifaa kama inavyofanya katika upotevu wa fedha. *(Makofi)*

(ii) Kamati inashauri Wizara ya Fedha, iunde kitengo cha kushughulikia potevu za fedha na vifaa vya Serikali. Kitengo hicho kifanye kazi kwa karibu sana na *PSRC* ili kupata taarifa mapema za madeni yanayodaiwa na Serikali kabla hata zoezi la kubinafsishwa kwa Mashirika ya Umma halijafanyika. Hatua hii itasaidia kufuatilia na kudai madeni hayo kabla shirika halijabinafsishwa.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, naliomba Bunge lako Tukufu likubaliane na mapendekezo haya ya Kamati ili kuweza kuridhia azimio la kumwezesha Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kufuta au kusamehe madeni au hasara itokanayo na potevu za fedha na vifaa vya Serikali yenye jumla ya shilingi 47,821,492,120.3 kama ilivyoainishwa kwenye taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati yangu, naunga mkono hoja na ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wote, waunge mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. GRACE S. KIWELU - MSEMAJI WA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, MIPANGO NA WIZARA YA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi hii ili niweze kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, kimsingi Kambi ya Upinzani, inaliunga mkono Azimio la Kumwezesha Waziri wa Fedha, kufuta au kusamehe madai au hasara itokanayo na upotevu wa fedha au vifaa vya Serikali kwa mujibu wa kifungu cha tano cha Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Fedha au vifaa vya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono kwetu, Kambi ya Upinzani ina ushauri ufuatao: Ukiangalia Mikoa ambayo inaombewa kufutiwa kutoka 1999/2000, 2001/2002 hali inatisha. Kwa mfano, Arusha shilingi 1.6 billioni, Dar es Salaam shilingi 1.1 bilioni, Mbeya shilingi 8.6 milioni, Mwanza shilingi 1.3 bilioni, Mara shilingi 1.4 bilioni na kadhalika. Ukiangalia mchanganuo wa wadaiwa, ni dhahiri kuwa wengine wamekufa na wengine wamefilisika lakini wapo wengine ambao wamebadilisha biashara lakini ni Wakurugenzi wale wale kwenye Makampuni mengine.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inasisitiza kuwa, Wizara iunde Kitengo Maalum kitakachofuatilia madai haya na Bunge lipewe taarifa kwa kupitia Kamati ya *PAC.* Aidha, Maafisa Wahasibu lazima wajitahidi zaidi katika kusimamia mapato na matumizi ya Serikali, aidha, wajitahidi kujibu hoja za ukaguzi kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, malimbikizo ya kodi yalikuwa hayajakusanywa, chini ya *PSRC* peke yake ni shilingi 12.5 bilioni kutoka asasi mbalimbali kwa mfano, *Tanzania Central Tender Board, Tanzania Tea Authority, Kilimanjaro Hotel Moreunsult, Print Park, Polysalts Co.Ltd., National Chemical Industries, National Engineer Co. Ltd., Tanzania Elimu Supplies* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ina wasiwasi kuwa *PSRC* hawajafanya juhudi ya kutosha ya kukusanya maduhuli haya, kwa hiyo, tunashauri kuwa, Waziri muhusika wa Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji, atoe maelezo ya kina juu ya hatua inayochukuliwa kudhibiti ukwepaji wa malipo ya mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Nina wasemaji wafuatao ambao nitawaita kwa mpangilio nitakaoutaja: Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, Mheshimiwa Aridi Uledi, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Edson Halinga na Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa. Orodha imefungwa. Namwita Mheshimiwa Abdillahi Namkulala.

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya awali kuchangia hoja iliyoko mbele yetu, kama alivyotuomba Makamu Mwenyekiti wa Kamati husika kwamba, tuunge mkono hoja, mimi ni mmojawapo wa kuunga mkono hii hoja. *(Makofi)*

Lakini kuna mawili, matatu ni bora nichangie. La kwanza ni kushangaa kwamba miradi ya maendeleo huko huko Mwanza, huko huko Arusha, huko huko Mara, kwa Mheshimiwa Spika na madume kuchukua fedha na kusamehewa huko huko. Sasa hili mimi sielewi, naomba lirekebishwe jamani Serikali huko. Kusini huku vilevile basi tuwekeni kwenye nafasi huku na sisi tuzoe hizi fedha mtusamehe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, lakini kuna potevu nyingine namwomba Mheshimiwa Waziri, awe mwangalifu katika kusamehe kwa mfano fedha zilizokusanywa lakini baadhi

zimepelekwa benki na baadhi hazikupelekwa, kwa nini hazikupelekwa au upotevu wa kwamba nyaraka za matumizi hazikukamilika au hazionekani, maana yake nini? Vilevile kuna mtindo mwingine wa midume kupewa fedha za *imprest* mamilioni kwa mamilioni ikafikia wakati wa kustaafu ndiyo kumsahau, ninyi mkampa mafao yake yote akaondoka na kuanza kumtafuta nyuma huku, inaeleweka hiyo? Fedha kuzoea mkajua kwamba, huyu anadaiwa anastaafu mkampa mafao yake yote baada ya miaka mitatu ndiyo kuanza kumtafuta, haonekani tufute madeni ahaa!. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa naiomba Serikali, nchi hii ni yetu sisi sote na hakuna mwenye dalili ya kwamba anataka kuhama nchi hii. Kwa hiyo, kufanya vizuri kama alivyofanya Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, mimi namshukuru bwana huyu, nchi sasa hivi ina sura kidogo, basi wangepatikana watu kumi au kumi na tano wa aina hii, mambo yangekuwa mazuri zaidi. Lakini tulio wengi sisi tukipata nafasi ni kuzoea fedha na kufanya utaratibu na mipango ili ufutiwe madeni.

Kwa ujumla naunga mkono hoja ila tu naiomba Serikali na Mheshimiwa Waziri, awe mwangalifu, upotevu huu tunaotaka kuusamehe umepotea katika mazingira yapi? Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu ya ombi la Waziri wa Fedha kuweza kufuta upotevu wa fedha na vifaa.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba, mimi naridhishwa na jitihada ambazo Wizara ya Fedha, inafanya hasa kupitia Ofisi ya Mhasibu Mkuu, kusimamia matumizi ya fedha za Serikali. Lakini bado inaonekana kuna mianya au namna isiyoridhisha kwenye baadhi ya sehemu na idara zetu za Serikali ambako usimamizi wa fedha za Serikali bado unalegalega sana.

Mheshimiwa Spika, ukitazama kwenye kitabu hiki ambacho tumepewa, kwa mfano, ukurasa wa kwanza kuna upotevu wa fedha ambao unaombewa kufutwa hapa wa zaidi ya shilingi milioni 166 ambao ulisababishwa na mhasibu katika Ofisi ya Ubalozi wetu nchini Uingereza. Huyu mfanyakazi alikuwa ni Mtanzania na nina uhakika hawa wafanyakazi ambao wanakwenda kufanya kazi kwenye ofisi zetu za Ubalozi, wanafanyiwa *vetting.* Sasa nashindwa kuelewa ni namna gani kwamba, huyu mtu inaelezwa katika taarifa hii kwamba, baada ya wizi kutokea huyu Mtanzania ametoroka. Sasa wasiwasi wangu mimi ni kwamba, isijekuwa kwamba fedha hizi zinakuwa zinaibiwa kwa kushirikisha watumishi wa Ubalozi na Viongozi wa Ubalozini na kisha kumshauri huyu mtu aweze kutoroka au kwenda sehemu nyingine ambako hawezi kuonekana, kwa sababu mimi siamini kwamba, Mtanzania anaweza kufanya kosa hili na akapotea akiwa ndani ya Uingereza asiweze kupatikana na akarejea nyumbani asiweze kupatikana. Kwa hiyo, mimi nilitaka maelezo ya Waziri ni namna gani anakubaliana na hili kwamba, linawezekana leo likaja kuombewa kufutwa hili ombi la Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje kwa mtumishi ambaye angeweza kufikishwa kwenye vyombo vya Serikali akaweza pia kuwajibishwa.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa pili kwenye hii taarifa kuna upotevu mwingine wa fedha kwenye ofisi za Ubalozi kwamba, baada ya ofisi za Ubalozi kwenye ofisi zetu za The Haugue na Paris kufungwa, kuna fedha ambazo zimetumika ambazo nyaraka hazionekani. Inaniwia vigumu sana kuamini kwamba, hili linawezekana. Kama ofisi inafungwa moja ya vitu vinavyotunzwa ni nyaraka mbalimbali ambazo zimekuwa zikitumika katika ofisi hizo. Sasa inakuwaje leo tunaambiwa kwamba, nyaraka fulani fulani ambazo zilihusika na matumizi fulani ya fedha katika ofisi hizi za Ubalozi zimeshindwa kuonekana? Ninashindwa kuelewa kwa sababu haiwezekani tukawa na uzembe wa namna hii na hakuna watu wanaowajibishwa. Kwa hiyo, sikubaliani na hili azimio kwa misingi tu kwamba, hatuelezwi ni hatua gani ambazo wanachukuliwa hawa watumishi wa Serikali, ambao wanafanya matumizi na ubadhirifu huu wa fedha za walipa kodi wa nchi hii. Kwa hiyo, inaniwia vigumu sana kusema kwamba, naunga mkono hoja, naunga mkono hoja bila kuelezwa ni hatua zipi zimechukuliwa?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilitaka tu Waziri anieleze hawa watumishi ambao walihusika na matumizi haya ambayo haikuambatana na *voucher* au *proper vouching* walichukuliwa hatua gani?

Mheshimiwa Spika, ukipitia hii taarifa ambayo tumepewa kuna kitu kimoja cha kusitikisha kidogo kwamba, kuna baadhi ya kesi ambazo naziona kabisa kwamba, zina ushahidi, kwa mfano, watu wamekamatwa wana fedha au wamejaribu kughushi fedha za Serikali lakini kesi zao zinapopelekwa Mahakamani, watu wale wanaachiwa. Sasa nadhani hii pia tunapozungumzia suala la kupambana na rushwa tunasema mhimili wa tatu kwa maana Idara ya Mahakama nayo imekuwa ni msumali mkubwa sana kwenye ubadhirifu wa fedha na mali ya umma. Baadhi ya Mahakimu ambao siyo waaminifu wamekuwa wakishirikiana na hawa wezi kuweza kukwepa mkono wa sheria. Kwa hiyo, nilikuwa nasema kwamba, bado tuna njia ndefu ili tuweze angalau kuisaidia Serikali yetu tuweze kupunguza uvujaji wa hili pato la Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukisoma taarifa hii pia ukurasa wa pili kuna eneo ambalo Wizara ya Ulinzi, walinunua maharage na baadaye maharage haya yakaonekana yana matatizo na hayafai kwa ajili ya matumizi ya binadamu. Lakini haikuelezwa ni hatua gani zilichukuliwa dhidi ya hawa waliohusika na ununuzi huu kwa sababu kwa taratibu za kawaida ununuzi wa huduma za vifaa kwa matumizi ya Idara za Serikali unafuata utaratibu wa zabuni. Kwa sababu ununuzi unafuata utaratibu wa zabuni kwa maana hiyo ni kwamba, huyu mzabuni alitakiwa awajibishwe ambaye aliliuzia jeshi maharage mabovu. Lakini hapa haikuelezwa, imeelezwa tu kwamba, baada ya bwana afya kupima maharage yale na kuyakuta kwamba hayafai kwa matumizi ya binadamu, yaliamuliwa yaende kutumika kwa ajili ya matumizi ya wanyama na kisha yalipopelekwa kwenye Kambi ya Jeshi Ruvu kwa ajili ya matumizi ya wanyama, bado yakaonekana hayafai pia hata kutumika kwa ajili ya matumizi ya wanyama. Sasa tunajaribu kujiuliza iliwezekanaje huyu mzabuni akauza maharage ambayo hayawezi kutumika kwa wanadamu na hata kwa wanyama na hakuna hatua zozote ambazo zimeelezwa zimechukuliwa dhidi ya huyu mzabuni? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa hayo machache ambayo nimezungumza, nilitaka tu niseme kwamba, wakati tukikataa kwamba kazi hii ya ufutaji wa madeni iwe inapita Bungeni, inatusaidia sisi Wabunge kuona ni namna gani Serikali inachukua hatua kusimamia matumizi ya fedha za Serikali. Kwa sababu vitu kama hivi kweli kabisa tusingeweza kuvifahamu. Lakini mimi nilikuwa namshauri Waziri wa Fedha kwamba, asitumike kuwa daraja la ufutaji wa matumizi ambayo yamesababishwa na ubadhirifu na uzembe wa watumishi wa umma. Kwa hiyo, zichukuliwe hatua angalau basi tuelezwe kwenye jedwali hili, kwa mfano, kwenye masuala haya niliyotaja ambayo yametokea kwenye ofisi zetu za Ubalozi tuweze kuelezwa ni hatua zipi zimechukuliwa dhidi ya watumishi waliohusika na matumizi haya ya ubadhirifu wa hizi fedha.

Lakini pia kwenye suala hili la maharage ambayo yalinunuliwa mabovu yaliletwa na huyu mzabuni, huyu mzabuni alichukuliwa hatua zipi na Serikali kwa kitendo cha kuuza maharage ambayo yalikuwa hayastahili na yalikuwa hayapo kwenye kiwango cha kuweza kuliwa na binadamu na wanyama kama ilivyoelezwa katika hii taarifa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hivi vipengele vilivyobaki, nadhani sina matatizo makubwa upande wa marekebisho ya vitabu, jedwali hilo nadhani sina tatizo nalo. Kwa upande wa maduhuli ambayo yameshindikana kukusanywa sina tatizo nalo. Lakini hapa katika hotuba ya Mheshimiwa Naibu Waziri, hapa amezungumzia kwamba, kuna baadhi ya mashirika ya umma ambayo yameuzwa na wale waliouziwa haya mashirika ya umma, kuna baadhi ambao hawajaweza kulipia madeni yao. Sasa inanipa tabu kidogo kuelewa ni kwa nini basi tumefika mahali ambapo tumeuza mashirika na tumewauzia watu ambao wameshindwa kulipa na bado tunaomba hii *provision* ya kuwafutia haya madeni. Nadhani labda Waziri, angetueleza wana mkakati gani kuhakikisha kwamba, kwa wale ambao wameuziwa mali za Serikali na wameshindwa kulipa kuna hatua madhubuti kabisa ambazo zinachukuliwa kuhakikisha kwamba, mali hizi hazitolewi bure na badala yake haya madeni yanakusanywa, tupewe mkakati kwamba, tusije tukafika mahali ambapo tutakuwa tunagawana mali za Serikali kwa utaratibu huu wa kuleta maombi ya kufuta vitu vya Serikali.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hoja hii ya Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kutoa pole kwako, Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, familia na ndugu na Wananchi wa Ulanga Mashariki, kufuatia kifo cha Mbunge mwenzetu, Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos James Kasapira, ambaye alifariki hapa Dodoma wakati wa Mkutano huu wa Bajeti. Namwomba Mwenyezi Mungu, aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi. *Amen.*

Mheshimiwa Spika, nikianza mchango wangu kwenye azimio lenyewe, naomba niseme tu kuwa, maelezo ambayo ameyatoa Naibu Waziri, mimi ninayakubali kwa kuangalia vyanzo vya hasara na potevu, juhudi ambazo zimefanyika hadi sasa mimi

naamini kabisa kuwa sababu ambazo zimetolewa ni za msingi hivyo kuhalalisha potevu/hasara hizi kufutwa. Hasara na potevu zingine ni za miaka ya 1990 kwa hiyo, ni za muda mrefu. Hivyo, kuendelea kuwemo kwenye vitabu vya mahesabu, nadhani siyo sahihi. Aidha, wahusika wa hasara hizo wengine wamefariki, wengine wamekimbia na hawaonekani. Kwa hiyo, hakuna haja ya kuendelea kuweka kwenye mahesabu hasara hizo hivyo ni sahihi kwamba zifutwe.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa na mwakilishi wa Kamati ya *PAC* kuwa, sehemu nyingine ni ile ya Serikali kushindwa kukusanya maduhuli na mapato kwa sababu mbalimbali, aidha, mashirika mengine yamefilisika na makampuni mengine hayako hivi sasa kwa hiyo, imeshindikana kabisa kukusanya kodi na mapato mengine ya Serikali. Kwa hiyo, kwa sababu hiyo sidhani kama kuna umuhimu wowote wa kuendelea kuweka mahesabu hayo kwenye vitabu vya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha Serikali kufuta hasara au potevu hizi haina maana kuwa hapo ndiyo mwisho wa wizi huo au hasara hizo na hasa kama bado kesi ziko Mahakamani. Serikali inawajibika kufuatilia kesi zilizoko Mahakamani hadi mwisho ili wahusika waweze kurudisha vifaa vya Serikali na fedha za Serikali pale ambapo inawezekana. Kwa hiyo, tunasisitiza kuwa zile kesi ambazo bado ziko Mahakamani, juhudi zifanyike kuhakikisha kuwa, kesi hizi zinakwisha na hasara hii inarudishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha hasara hizo zinarudishwa lile suala la kuwa na kitengo maalum cha kufuatilia hasara au potevu zote hizi ni muhimu sana. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali, kuwepo na kitengo maalum ambacho kitakuwa na kazi ya kuhakikisha hizi hasara ambazo tunazifuta pale ambapo inawezekana, basi fedha hizo zinarudishwa na wahusika wanalipa vifaa ambavyo wamevipoteza. Kwa hiyo, hii isiwe mwisho wa kufuatilia kesi zote ambazo ziko Mahakamani na kuwatafuta wale wote ambao wametoroka ambao wamesababisha hasara mbalimbali, hii tunaruhusu ifanyike ili kuhakikisha vitabu vya mahesabu ya Serikali vinasafishwa. Tungependa taarifa juu ya potevu hizi za nyuma ziwe zinaletwa Bungeni, mara kwa mara ili tujue hali halisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa na mchango mdogo na baada ya mchango huo niseme tu ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na mwisho kabisa nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Vilevile nachukua nafasi hii kuipongeza Ofisi yako ya Bunge, kwa kusimamia vizuri sana mazishi ya Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira na Waheshimiwa Wabunge kwa ushiriki wao. *(Makofi)*

Kwa kweli imetusaidia na kwa kweli imetupunguzia majonzi. Kamanda amekuja amepigana na ameshinda vita amepumzika. Mungu amuweke mahali pema peponi. *Amen.*

Mheshimiwa Spika, hapa tupo kwa mujibu wa Sheria Na. 43(1), sheria hii ya usimamizi wa udhibiti wa fedha za umma za mwaka 2001 za Bunge kwamba, sasa linashirikishwa katika kufuta madeni ya nje. Haya yalikuwa ni malalamiko ya muda mrefu sana tulidhani wanafuta tu, kumbe yako mambo ambayo mmejitahidi kuyafuatilia. Nilikuwa naangalia katika Jedwali Na. 1, potevu za fedha za vifaa vilivyotajwa katika Jedwali Namba 1, vipengele 93, viko vingine ni kwamba *cash* ambazo zilipotea kwa hiyo, walijitahidi Public Accounts Committee mmekubaliana kwa hiyo, mmekubaliana mkaleta Bungeni na mimi nakubaliana na ninyi. Kifungu B mapato ya maduhuli ambayo yameshindikana kukusanywa fedha zimetajwa jedwali Na.2 kuna vipengele 19 na Public Account Committee wamekubaliana na mimi naunga mkono. Kipengele namba (c) usawazishi wa kumbukumbu katika vitabu fedha zimetajwa, kuna Jedwali Na. 3 vipo vipengele kumi. Nimeona kwenye jedwali mmeweka taratibu nzuri tu mkaweka jedwali mkaonyesha kama ni *cash* au *store, expenditure, unvouched* na nikaona kwamba na kiasi chenyewe kilichokuwa kimeweka pale. Hii nimekubali sana na nashukuru sana. Lile jedwali la tatu mmeweka *adjustment* ni kweli unakata pua kuunga wajihi ili kusudi hesabu zenu zikubaliane. Huu ni utaratibu wa *financial regulations,* ambazo zimetungwa ili kuona kwamba Bunge linashirikishwa. Tunashukuru sana kwa hilo.

Kwa mfano, kuna mengine kwa mfano, kifungu namba 43, unakuta mtu anadaiwa vitabu shilingi 75,000 yuko Shaicom, ambaye ameshaacha shule mwaka 2001. Sasa mtu kama huyu kweli kumfuatilia unashindwa kwa hiyo inahesabu mahesabu. Ila la msingi kama haya, kwa sababu madeni yenyewe yanaishia mwezi Juni, 2003 kwa hiyo kuwe na mawasiliano ya kuhakikisha kwamba, wale watu ambao wanawadai hayo tunayafuta wasije wakadai halafu wakaingiza mfukoni mwao. Maana tunafuta leo hapa lazima kuwe na mawasiliano hayo kwa sababu ni Juni tu si ajabu kuna baadhi ya vipengele fulani wanafuatilia haya madeni. Wakisikia tumefuta wanajua sasa inakuwa *(OC)* ya chakula watafuatilia hizi kwa nguvu zote watagombea haya madeni watafanya michanganuo nao vilevile. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa hilo nilikuwa nasema hayo natoa tahadhari hiyo, *Public Accounts Committee next time* vilevile tuambie madeni mangapi mliyoletewa pale halafu mangapi ambayo ninyi mliyakata wafuatilie na yale yalitakiwa yafutwe kupitia Bunge, kuwe na kipengele kingine kinachoonyesha ili *Public Accounts Committee* pengine wanasema deni hili linawezekana, hili haliwezekani ili kusudi tuweze kujua. Kwa sababu, inaweza ikaonekana kwamba, madeni mengine yanaweza yakawezekana kwa utendaji wao wakatoa visingizio kwa hiyo, watu wakaanza kuyadai baada ya kufuta. Kwa hiyo, mnadaiwa madeni haya mtafuatilia kwa kutumia tovuti za Hazina au simu namba ambayo wameiandika kwenye hili jedwali kwamba mmefutiwa madeni haya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niseme yale ninayoyaona hapa.

Mheshimiwa Spika, upotevu huu ni mkubwa sana na unaonyesha jinsi tunavyojirudisha nyuma kimaendeleo. Kama upotevu huu unaachiwa mwanya, hatutakwenda mahali popote kwa sababu fedha zinazopotea ni nyingi kuliko zinazotumika kwa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nadhani liko tatizo ama la Serikali au la Wizara. Hawa wanaoiba fedha za Serikali wanazitumia kwa kitu gani? Wengi wanajengea nyumba, wananunua magari na vifaa mbalimbali. Hivi kwa nini wasifilisiwe? Sijaona hatua yoyote inayotumika kuwafilisi hawa watu na wizi huu hautokei kwa dharura, ila wanatumia muda mwingi tu. Chukua kwa mfano, Ruvuma, *Vote* Namba 82 watu wamelipana mishahara zaidi miaka karibu minne.

Hivi kweli Ukaguzi ulishindwa kugundua hali hii kama sio ujanja tu? Maana maneno yaliyoko huko nje, watu wanasema Wakaguzi wakienda pale kwanza, wanatunzwa vizuri ili wasahau. Hii inaonyesha ni kweli, ndio maana mambo haya yanakwenda namna hii. Miaka yote mtu analipwa mshahara zaidi ya kiwango chake, Ukaguzi haujaona. Hivi maana yake nini? Nadhani liko tatizo hapa, ni vizuri Wizara ya Fedha kwa kweli irekebishe na iwe na uchungu wa hela kwa maendeleo yetu.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba, kila Idara ina Mkaguzi wa Ndani. Hivi kazi ya Mkaguzi wa Ndani ni nini? Si a-*pre-audit* yale yote yanayotokea kwa kila siku na matumizi? Sasa hela zinatumika miaka miwili, mitatu, hajagundua, hivi ana kazi gani pale? Tunamwajiri wa nini huyu, maana hata hasaidii wala haleti msingi wowote wa kuokoa hela za Serikali? Mimi nadhani iko haja ya kuona kwamba, kwa kweli hawa Wakaguzi wa Ndani hawana sababu kuwepo, maana wangekuwa kila siku wanagundua na wanaona kila vocha inayotolewa pale wanatoa sababu mapema na upotevu huu usingeweza kutokea. Lakini wamekaa kimya miaka yote hela zinakwenda, mpaka Mkaguzi Mkuu apite ndipo tujue kuna hasara, maana yake nini? Kwa nini tumeweka watu, pengine hawana ujuzi na pengine ndio njama, tumeweka watu kula hela za Serikali kwa kutegemea zitafutwa hakuna atakayepata hasara. *(Makofi)*

Mimi nadhani hapa tuangalie hawa Wakaguzi wa Ndani, maana hakuna sababu ya kuwa na sehemu hiyo ya Wakaguzi wa Ndani, tunapoteza bure hela zetu na muda usioeleweka.

Halafu kuna fedha zinapelekwa kule, mimi nadhani ipo njama fulani. Katika utaratibu wa pale Wizarani sio rahisi mtu kuiba hela. Lakini ilitokea Wilayani kwangu, hela zimetolewa Wizarani zikaletwa kule mishahara ziada. Kufika kule wakafuata watu wa Wizarani huko watumishi kuja kugawana zile hela. Bahati nzuri tukagundua tukatoa taarifa hiyo. Sasa hawajaniambia kama hatua zimechukuliwa vipi. Inawezekana hizo nazo zikaletwa mwaka kesho kufutwa. Sasa tusipozingatia taratibu hizi za kujali fedha na utaratibu, hatutakwenda mahali popote.

Mheshimiwa Spika, kuna hizi *reallocation* zinazofanyika. Ni kweli Waziri ana-*reallocate* fedha kutokana na matatizo hata hizi za shughuli za njaa. Hivi kweli hela hizi zote tunahakikisha zinatumika sawasawa? Maana inawezekana mambo mengine haya

tunafanya kwa kuwapa watu mwanya kujitajirisha na kujinufaisha. Ni vizuri tuwe waangalifu wa kuangalia. Kuna miradi mingine kama mradi huu wa mabasi ya kwenda kasi, hela zimetolewa, nani asimamie, Manispaa, si Serikali hiyo hiyo? Hapa hapa hela zimetolewa za mabasi ya vijana, zimeliwa mpaka leo. Leo tunasema tuanzishe Mradi wa Mabasi Dar es Salaam, kweli utadumu huu?

**MBUNGE FULANI:** Haudumu.

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Ni nani anayependekeza mambo haya, mabilioni ya umma yaende yaanzishe mradi ambao nina hakika hautafanikiwa? Wale Waswahili Mjini wanatuambia sisi wanasema acha Serikali na ilete, sisi tutahakikisha inakufa. Sisi tuna vipanya vyetu humu, halafu walete hayo mabasi, tule wapi? Wanasema hivyo na mradi huu kwa kweli hauna matumaini ya mafanikio. Hizi fedha tusipoangalia zitapotea katika msingi huo. *(Makofi)*

Fedha hizi labda kama ufuatiliaji utakuwaje, sijui Serikali ikubali kuingia katika mkataba wa kufanya biashara, ndipo tuelewe hivyo. Nadhani ziko tenda zinafanyika, lakini mambo yanayofanyika kule hayaeleweki wala majibu hayapatikani. Kama yaliyotangazwa kwenye magazeti na kwenye *TV* huko lakini hakuna majibu, sasa kama watu hawa wa tenda sio waaminifu wa kuzingatia haya mambo, hela zinapangwa hazitumiki inavyopasa tunanyamaza tungoje kuja kufuta, hivi tutakuwa hatuhusiki katika kupata faida ya fedha hizo? Mimi nadhani watu wanaopewa au kukabidhiwa kusimamia fedha hizi hawana uaminifu, iko haja ya kuwachunguza zaidi wale tunaowakabidhi madaraka ya kusimamia fedha zetu, vinginevyo hatutakwenda hata kidogo, tutabaki na hasara tupu.

Ukiangalia hata kwenye majedwali haya, wameandika tu amepotea, haonekani alipo. Hivi nchi hii mtu amepotea haonekani aliko. Wapi? Hawa Wakenya mbona wamepatikana, hawa wa fedha za Hazina zetu ndio hawaonekani, wamekimbilia wapi? Ni mbinu tu ya kutulaghai kula hela na kufanya maendeleo yetu yakwame. Hili nadhani Waziri wa Fedha, alione na Ukaguzi uwe karibu zaidi. Kila anapopatikana mtu achukuliwe hatua za mara moja, itatusaidia sana. Kama mtu amechukua hela afilisiwe hata ukoo wake maana umeshiriki kula hizo hela. Wafilisiwe turudishe fedha zetu, ndipo watu watakapoelewa kwamba, kwa kweli kuchezea hela za umma hakuna mchezo. Tutakwenda, vinginevyo hatuwezi kwenda mahali popote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hili limetendeka, sasa tufanye nini? Tunaunga mkono lakini kwa kweli kuwe na mabadiliko. Iwe ni mara ya mwisho ya kukubali kirahisi rahisi haya kufutwa. Tusingependa itokee tena mwakani kufuta kwa matumizi ambayo ni ya ulaghai, ujanja ujanja huu, tusiukubali hata kidogo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA:** Mheshimiwa Spika, natanguliza shukurani zangu za dhati kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia katika Wizara hii.

Ninashukuru ni hoja nzuri ya kufuta, wanasema ukifutiwa na wewe futa. Sasa tumeshafutiwa na Wazungu huko, lazima na sisi tufute. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, nadhani isiwe mwendelezo huu ya kwamba ukishafutiwa tutakuja kuchezewa ile tabia ya kuletewa sahani ya asante halafu mtu anakwambia imekufa utakapomkopesha. Kwa maana kwamba, unakuwa ni mchezo wa futa futiwa. Kwa hiyo, mimi naomba tu niitahadharishe Serikali kwamba, ni vyema pia kumfutia unapoona kuna sababu ya muhimu, sio kufutiana.

Kwa mfano, ukiangalia katika hii *Sub Vote 46* unaambiwa mtu ameiba lakini ushahidi unasema ameachiwa huru. Ina maana huyu ni *ready-handed* halafu anapotelea mkononi, umemshika, anapotea. Kwa hiyo, hii inatia shaka kwamba, kwa kweli kuna haja ya kuwa makini, hii ni pesa ya Wapiga Kura wetu ambao ni jasho lao, sasa tukiwa sisi tunakaa huku tu Mswahili mmoja anakwenda anaibua shilingi milioni 100, shilingi milioni 200 kesho anasema sina, zimeliwa, kuna haja ya kuwa makini.

La pili, wasiwasi wangu ni hawa Wawekezaji. Kwa kweli Wawekezaji wanaobadilisha mmiliki ni lazima tuwe makini nao. Mtu anafanya biashara miaka mitatu, minne, akiona amefikia mahali anakimbia anabadilisha kampuni halafu anasema ana-*declare* kufilisika. Halafu sisi tunabeba mzigo. Kwa hiyo, sisi tutakuwa tunambebesha mwananchi mzigo ambao sio wake.

Mheshimiwa Spika, sasa zito linalokwenda ni hivi, tumefuta madeni, lakini Serikali inakumbuka kwamba, bado inadaiwa na *Mara Corp.* Kuna wakulima wameuza pamba yao miaka mingi mno zaidi ya miaka saba mpaka leo hii hawajalipwa na *Mara Corp.* ilikuwa chini ya usimamizi wa Serikali. Sasa nitaomba maelezo kwamba katika huu mtindo wa kufuta madeni, je na wale itakuwaje, watafutiwa au watalipwa?

Mheshimiwa Spika, halafu lingine ninaloomba pia niongelee ni kuhusu mradi wa uchimbaji madini wa Bulyankhulu na Geita. Mwaka 2003 tuliutembelea tukapata bahati ya kuingia mpaka huko chini ya machimbo tukapewa taarifa kwamba, kuna Mzungu mmoja alikuwa anamiliki pale. Baada ya kuwa amemiliki akamuuzia Mzungu mwingine huko huko Ulaya. Alipomuuzia huko Ulaya, yule Mzungu akaja alikuwa Marekani, lakini baada ya kuuziana wamerudi hapa yule Mzungu anasema ana deni analipa kwa yule Mwekezaji wa pili. Kwa maana hiyo ni kwamba mrabaha wa Serikali unakatwa na waliuziana kati ya shilingi bilioni mia moja na kitu. Sasa sisi Watanzania tunakatwa mrabaha wetu kwa sababu yule bwana analipa deni.

Mimi nilibahatika kufika pale, tumeangalia nikawa najiuliza aliuza nini kwa shilingibilioni mia moja na kitu? Nikakuta hakuna kitu, ni ardhi. Lakini sheria yetu inasema hatuuzi ardhi. Sasa waliuziana nini mpaka mrabaha wetu sasa ukatwe kwa kwenda kulipa deni? Kwa sababu tumeongelea madeni lazima tufafanue madeni yote. Sasa nitaomba ni kwa nini hatupati mrabaha wowote katika huu mgodi na ni kwa nini tunalipa deni ambalo wao wameuziana halafu wanakata tena kwenye mrabaha wetu. Kwa hiyo, nitaomba Mheshimiwa Waziri, anipe maelezo kwa sababu tunapoteza hela nyingi sana, shilingi bilioni mia moja na kitu ni nyingi mno kuweza kuzilipa kutokana na

mrabaha wetu kwamba wao waliuziana halafu wauziane deni watupe sisi, ndio tulipe! Kwa nini huyo mtu kama alikuwa wameuziana asiendelee kulipa kwa sababu sisi tunalipisha mrabaha kutokana na madini yetu, sio kutokana na kuuziana.

Mheshimiwa Spika, nadhani sina mengi zaidi ya hayo, naomba kusema kwamba, ninaunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):** Mheshimiwa Spika, naomba kuwashukuru wachangiaji mbalimbali wa Azimio hili nao nikiwataja kwa majina yao, wa kwanza ni Makamu Mwenyekiti wa *PAC*, Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa; Msemaji Mkuu wa Upinzani, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, Mheshimiwa Aridi Uledi, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Edson Halinga na mwisho Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa. Nawashukuru wote kwa michango yao katika hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza, nasema wazi kwamba, tunakubali ushauri wa Makamu Mwenyekiti wa *PAC,* pamoja na ule wa Msemaji Mkuu wa Upinzani na yale yote waliyoshauri pamoja na Wabunge wengine tutayachukulia hatua.

Lakini kabla sijaendelea kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, nakumbusha tena, wakati nawasilisha Azimio hili, nilisema kwamba, kwa mujibu wa Kifungu cha tano cha Sheria ya Udhibiti wa Fedha za Umma ya mwaka 2001, Waziri wa Fedha anayo mamlaka ya kusimamia na kudhibiti matumizi ya fedha za umma na kutoa taarifa Bungeni kama hasa mlivyotaka ninyi Waheshimiwa Wabunge, wakati tunajadili hoja hii mwaka 2001//2002.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 43(1), nimesema Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Fedha za Umma mwaka 2001, Bunge linaweza likatoa idhini kwa Waziri wa Fedha kufuta hasara itokanayo na upotevu wa fedha, vifaa vya Serikali, Madai ya Kodi pamoja na riba itokanayo na malimbikizo mbalimbali ya kodi. Hii ni *postmortem.* Kama nilivyokwisha sema hapo awali, Waheshimiwa Wabunge, mengi ya haya yametokea mwaka 1980 na mengine machache sana kabla ya kuwa na sheria hii ambayo inakuwa na Udhibiti bora zaidi kuliko ilivyokuwa hapo mwanzo. Ukiangalia huko nyuma, hata hivyo, utaona kazi ya Udhibiti imeboreshwa sana kwa sababu madeni yaliyokuwa yafutwe hapo kabla yalikuwa ni mengi zaidi kuliko madeni tunayoomba yafutwe hii leo na *PAC* imegundua hilo.

Pili, *PAC* imepitia hoja mbalimbali tulizozitoa, kwa nini upotevu huu ufutwe. Haya yanatokana na taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali na yale ambayo hayakukubaliwa yafutwe mwaka 2003/2004, ndiyo wamesema kwamba, mkayachukulie hatua zaidi. Tena ushauri wao mwingine ni kwamba, hayo tunayotaka yatoke kwenye vitabu vyetu, bado tusiyaache tu kwamba yamekwisha, bado tuendelee kuyatafuta lakini kwa sababu ya usumbufu, kuweka vitabu vyetu sawa, ni lazima upotevu huu ufutwe. Hata hivyo wakati Makamu Mwenyekiti anawasilisha ripoti ya Kamati, amesema zaidi ya shilingi bilioni mbili bado Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Mkaguzi na Mdhibiti

Mkuu wa Serikali, wakayafanyie kazi zaidi hayo mengine yaliyosalia ili wayalete hapa mwakani au tutakapokuwa tayari yapitiwe na *PAC* na kama *PAC* itakubali waweze kuyafuta.

Mheshimiwa Spika, sasa nakwenda kwenye hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, nikianzia na Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, ambaye anashangaa kule kwenye miradi ya maendeleo ndiyo kwenye kusamehewa fedha, fedha zilizokusanywa nyingine hazikupelekwa Benki na aliyepewa *imprest* na baadaye anapoachishwa kazi *imprest* ile kwa nini asikatwe. Kwanza, kama nilivyoeleza kwenye utangulizi wangu wa kujibu hoja hizi, hoja hii ya madeni na maendeleo nadhani hakuna uhusiano wowote. Kwamba, kule kwenye fedha nyingi ndiko ambako kuna matumizi mengi au kuna upotevu mwingi. Kwa sababu Mikoa iliyotajwa ukiangalia hasa utakuta kwamba, ndiyo inayochangia katika ukusanyaji wa mapato, kwa mfano, Dar es Salaam pale Ilala, Arusha na Mwanza. Kwa hiyo, vigezo hivyo Mheshimiwa Abdillahi Namkulala vya kupanga miradi ya maendeleo na tofauti ya matatizo ya kukusanya mapato hayaendi kabisa na hayalingani na hoja yetu iliyopo hapa Mezani hivi leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, amezungumzia juu ya Balozi zetu mbili hizi, Ubalozi wetu wa London na Ubalozi wa *The Haugue,* ambao ulifungwa na kwamba hawa wafanyakazi ilikuwaje wasipatikane. Tunachosema ni kwamba, kama Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu, ameridhika kwamba, fedha ile hatuwezi kuipata tena, sisi lazima kwenye vitabu vyetu tufute fedha ile. Lakini si hivyo tu, kwa mfano, London, anayehusika kweli hayupo ameacha, ni Mtanzania kweli ambaye ameacha amehamia London siku nyingi na amefanya kazi siku nyingi sana pale. Lakini *records* zilipatikana zilikuwa fedha ni zaidi ya hizi zilizotajwa katika Jedwali Namba Moja kifungu cha saba kama sikupotea. Lakini zile ambazo hazikupatikana maandishi yake na stakabadhi zake na yote yanayohusika ili fedha zile zipatikane havipo, havipatikani na kwa sheria pale Uingereza walipotaka hata kumpeleka Mahakamani hata kama mmemtafuta, tungekuwa sisi hatuna cha kujibu kwa sababu *records* zinazohusika hazipo na hakuna sababu za yule mtu kushikwa. Atakwama kweli ikiwa ametafutwa na kweli bado yupo Uingereza lakini Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu, hakupata *records* zote zile ambazo *they can justify* na tukashinda kesi yetu Mahakamani kwa yule mtu aliyehusika.

Hivyo hivyo, kwa Balozi wetu wa *The Haugue* kwa sababu risiti na *records* nyingine hazipatikani, sisi kama ni Wadhibiti wa kusimamia fedha ya Serikali ni lazima tuseme kwamba, hii isikae tena katika Hesabu zetu za Serikali kwa sababu fedha hizi hazipatikani ndiyo maana tunaleta hapa kama mlivyoomba ninyi Waheshimiwa Wabunge. Ni kweli nikiri kwamba, hapo kabla hatukuwa na Wahasibu wazuri katika Balozi zetu, lakini sasa hivi tunajitahidi kufanya hivyo na hivi sasa Mhasibu aliyepo London ni Mtanzania, ametoka hapa hapa na ni *qualified* na tunaamini kwamba, *records* zetu zitakwenda sawa kama tulivyofanya kwa Balozi zetu nyingi vilevile. Kwa hiyo, kumkamata mkosaji, kisheria lazima uwe na ushahidi kamili kwamba amefanya kosa hilo.

Kuhusu Mahakama kuachia Wahusika nadhani ndiyo Mahakama na sisi hatuwezi kuingilia Mahakama. Kama uamuzi wa Hakimu ni huo, wala sithubutu kumtuhumu kwamba amekula rushwa. Sisi wajibu wetu kama Wadhibiti wa Fedha, linapotokea kosa lolote lile la fedha kupotea ni kupeleka katika vyombo vinavyohusika na hatua zinazofuata ndiyo wao wanazichukua, kwanza Polisi halafu Mahakama. Lakini kama Mahakama na Polisi nyingine hizi ni kwa sababu ushahidi unachukua muda mrefu, ndiyo pengine kesi hizi zinafutwa. Kwa hiyo, Mahakama ikishasema kwamba hizi fedha hazipatikani, sasa Wizara ya Fedha haiwezi ikasema kwamba fedha hizi bado zitakuwa katika vitabu vyetu. Kama nilivyosema awali, ndiyo maana tunaomba adha hii ituondokee. Lakini pale inapoyumkinika kama walivyotushauri Kamati ya *PAC,* tutakuwa bado tunaendeleza ili kama alivyoshauri Mheshimiwa Edson Halinga kwamba, zisije zikarudi nyuma zikaingia mifukoni mwa watu au Mheshimiwa Semindu Pawa, aliyeita Ofisi ya Chakula. Kwa hiyo, bado tutakuwa tunaendelea na kuhakikisha kwamba fedha hiyo haipotei.

Kuhusu maharage ya Jeshi, hatua zinazohusika zimechukuliwa. Kama nilivyosema, sisi Wizara ya Fedha, kama zimethibitishwa na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwamba fedha hizi kweli hazipatikani, ni wajibu wetu sisi kuomba kwamba, fedha zile zifutwe zisiwemo katika madaftari yetu. Jeshini watakuwa na hatua zao wenyewe za kumchukulia aliyehusika, lakini sisi hatukuwa na zaidi na kuripoti kama ilivyo hapa. *In fact* ukiangalia ripoti yetu ya mwaka huu namna tulivyoweka vifungu hivi, utaona kwamba, tumeendeleza kusema sana nini hatua iliyochukuliwa kwa kila kesi ambayo imejitokeza hapa.

Mheshimiwa Marwa pia aliuliza juu ya mkakati wa Serikali wa kudai fedha hizi. Fedha hizi kama nilivyosema, bado tutakuwa tunazifuatilia kwa zile ambazo zinaweza kupatikana, bado kesi nyingine tunaziendeleza. Kwa sababu hizi vilevile zilikuja mwaka 2003 zilikuwepo. Baada ya kufikia hatua tuliyofika, utakuta kitabu hiki kimetiwa sahihi haya maelezo ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, pamoja na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu kwa ushirikiano wetu, ili kuhakikisha kwamba, kweli lile jambo haiyumkiniki kwa pande zote mbili. Nakubaliana sana na Mheshimiwa Aridi Uledi, nashukuru umeliona hili kwamba hasara hii ilikuwepo toka *1990s.* Kwa sasa hivi kuna kitengo maalum ambacho kimesema kama alivyotushauri Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa *PAC,* pamoja na Msemaji Mkuu wa Upinzani. Hiki Kitengo kama mlivyotushauri wakati tunaizungumzia hoja hii, hili tunakubaliana nalo. *(Makofi)*

Kwa njia moja hapa nimeshakujibu Mheshimiwa Semindu Pawa, kwamba tunakuhakikishia kwamba, haitakuwa Ofisi ya Chakula, hata zikija tunashauriwa tufanye tu, suala hili tunaendelea kulifuatilia hili jambo na tutahakikisha kwamba tunakwenda kama tulivyokusudia.

Mheshimiwa Edson Halinga, amezungumza kwamba, watu hawa wanaohusika na wizi wa mali za Serikali wanakuwa na majumba, wanakuwa na magari, lakini bado wanaachiwa na hata huku mwisho unashauri kwamba, watu wale kwa nini basi wasichukuliwe hatua hata pia wasifilisiwe?

Mheshimiwa Edson Halinga, nadhani hata wewe hutakubali kwamba, kama amefanya kosa mwanao na mwanao hayupo uchukuliwe wewe ukashtakiwe. Wewe baadaye utasema hukufanyiwa haki, kwa sababu kama aliyefanya vitendo vibaya ni mwanao na bahati mbaya hana kitu na wewe una matrekta mawili, ndiyo uanze kuja matrekta yako, utakuja hapa hapa kupiga kelele tena. Nadhani hili si jambo la busara.

Lakini nakubaliana na wewe kuhusu Wakaguzi wa Ndani na nikiri kwamba, tulikuwa hatuna watu wengi ambao wana ujuzi wa kutosha. Sasa hivi tunajitahidi sana kuwa-*train* wale ambao wana ujuzi wa kutosha na kama haya yalikuwa yanatokea hapo zamani, kama nilivyosema kuanzia mwaka 1980, hii *postmortem* tunayoifanya nina hakika haitatokea kama ilivyokuwa inatokea hapo mwanzo. Kwa hiyo na sisi huo uchungu wa hela tunao vilevile kama ni Wadhibiti wa fedha za Serikali. *(Makofi)*

Ndiyo maana hayo yalikuwa yanafika miaka mitatu, miaka minne, lakini sina uhakika kwamba, kweli wachunguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, wanahongwa chochote, hilo sidhani kwamba linatendeka.

Lakini kama linatendeka, jambo zuri la kufanya hivyo ni kama ulivyofanya wewe, ulipogundua fedha zimekuja kule na baadaye wameita Maofisa waje wagawane, ukaripoti haraka na tukaliwahi. Hivyo ndivyo inavyotakiwa kila mtu afanye hivyo.

Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa, alizungumzia juu ya wawekezaji wanaobadilisha umiliki. Sasa hivi kuna timu. Hii ndiyo maana ya kuwa na timu ili hata ukibadilisha biashara yako, maadam una timu na jina lako lile lile, bado tunaweza kukufuata na kuhakikisha tunapata mali yetu.

Lakini hili la mwisho nadhani uonane na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, kuhusu Bulyankulu, waliuziana na wakachukua mrabaha wenu wasikupeni ninyi, itakuwa hilo ni jambo la busara na atakupa mawaidha yaliyokuwa mazuri zaidi na ushauri ulio bora ili kupata *royalty* yako.

Mheshimiwa Spika, baada ya kujibu hoja hizo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la kumwezesha Waziri wa Fedha kusamehe au kutufa madeni liliridhiwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja inayohitaji uamuzi ni ile ile iliyopo kwenye *Order Paper,* kwamba Bunge lipitishe Azimio la kumwezesha Waziri wa Fedha kufuta na kusamehe madai au hasara itokanayo na upotevu wa fedha au vifaa vya Serikali kama ilivyoainishwa kwenye Azimio lenyewe. Bunge limepitisha Azimio hilo la kumwezesha Waziri kufanya mambo hayo. *(Makofi)*

Mpaka hapo Waheshimiwa Wabunge, ndiyo tumefikia mwisho wa Kikao cha asubuhi.

Kwa hiyo, sasa nitasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni, tutakaposikiliza hotuba ya Waziri Mkuu ya kufunga Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge.

*(Saa 5.38 asubuhi Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**KATIBU MEZANI - NDUGU JAPHET M. SAGASII:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba shughuli zote zilizokuwa zimepangwa kwa ajili ya Mkutano huu wa Kumi na Sita, sasa zimemalizika. *(Makofi)*

## KUAHIRISHA BUNGE

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu leo limehitimisha kazi zote zilizokuwa zimepangwa kwa ajili ya Mkutano wa Kumi na Sita. Kabla ya kuendelea na maelezo yangu naomba nami niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa rambirambi zangu kwa wananchi na familia za Marehemu Yete Mwalyego aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini na ya Marehemu Kapteni Theodos Kasapira aliyekuwa Mbunge wa Ulanga Mashariki, kutokana na vifo vya ghafla vya wawakilishi wao vilivyotokea hapa Dodoma wakati wanahudhuria Mkutano huu wa Kumi na Sita wa Bunge lako tukufu.

Marehemu hawa walikuwa viongozi hodari na waliotoa michango mikubwa katika maendeleo ya Majimbo yao na nchi yetu kwa ujumla. Tunamwomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu wetu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, kazi ya Ubunge ni ngumu, yenye fadhaa *(tension)* kubwa na inayohitaji uvumilivu wa hali ya juu. Hii ndiyo hali ya kawaida ya kazi hii, lakini fadhaa huzidi jinsi kipindi cha Ubunge kinavyoelekea tamati yake. Aidha, vikao vya Bunge navyo hukaa kwa saa nyingi na kama Mkutano ni mrefu kama huu wa bajeti, basi hali hiyo yaweza kabisa kuathiri afya za Waheshimiwa Wabunge. Pamoja na madhara ya kazi yenyewe ya Ubunge, itasaidia sana afya zenu Waheshimiwa Wabunge kama tutazingatia baadhi ya mambo mengi haya matatu muhimu:-

- Kupima afya zetu mara kwa mara. Hili linashauriwa sana ili ujue afya yako, kama una kisukari, shinikizo la damu, mafuta mwilini na dhadhalika. Huduma hii inapatikana hapa Bungeni.

- Kufanya mazoezi ya viungo. *(Makofi)*

- Kula aina na viwango vya vyakula vinayoshauriwa na wataalam kutokana na umri na hali ya afya ya kila mmoja wetu.

Tunakoelekea fadhaa zitazidi kuwa kubwa, hivyo tufuate ushauri huo. Hii siyo tukiwa Dodoma tu bali hata katika Majimbo yetu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya muda wa takriban miezi miwili ya kuwa nje ya Majimbo yetu ya uchaguzi, bila shaka Waheshimiwa Wabunge tuna hamu ya kurejea kwenye Majimbo yetu kukutana na wapiga kura na vile vile kuwaeleza maamuzi yote yaliyofikiwa katika Mkutano huu. Katika Mkutano huu kama ilivyo kawaida, Bunge limeridhia na kupitisha Bajeti ya Serikali na Mpango wa Mwaka 2004/2005. Aidha, Makadirio ya Matumizi ya Wizara zote yamepitisha. Jumla ya maswali 403 ya Waheshimiwa Wabunge yakiwemo mengine mengi ya nyongeza yaliweza kujibiwa na Serikali. Vile vile Miswada minne imepitishwa, mingine minne kusomwa mara ya kwanza na Maazimio mawili kupitishwa.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya Serikali ya mwaka 2004/05, ambayo tumehitimisha majadiliano yake imelenga kukusanya mapato ya ndani yasiyopungua asilimia 13.8 ya pato la Taifa. Ili kufanikisha lengo hilo, Serikali imeelezea makusudio yake ya kutekeleza hatua kadhaa za kurekebisha mfumo wa utawala wa kodi mbalimbali hususan mfumo wa kodi ya mapato, kodi ya ongezeko la thamani, ushuru wa bidhaa na forodha, kodi za leseni na kadhalika. Lengo la marekebisho hayo ni kupanua wigo wa kodi, kudhibiti ukwepaji kodi, kuondoa kero za kodi na kutoa unafuu mkubwa kwenye kilimo na shughulli za biashara pamoja na kuongeza ufanisi katika mamlaka zinazosimamia kodi nchini. Aidha, pamoja na kusimamia ukusanyaji mapato, Serikali imedhamiria kudhibiti matumizi yake kikamilifu. Napenda kusisitiza kuwa hatua hizi za utekelezaji wa sera za Serikali ni hatua madhubuti na fursa ya pekee ya kuwawezesha Watanzania walio makini na wenye nia thabiti ya kupenda kujiendeleza, kuongeza uzalishaji mali na kufanya biashara halali ili kupambana na umaskini na kujiletea maendeleo kwa haraka. Changamoto kubwa iliyo mbele yetu ni kwa wakulima, wafugaji, wavuvi, wawekezaji, wafanyabiashara ndogo na za kati na wananchi wote kwa ujumla ambao ndio walengwa wakuu wa bajeti hii kuwa wabunifu, kufanya kazi kwa bidii, tija na ufanisi ili kuwezesha uchumi wetu kukua kwa viwango vya juu zaidi. Serikali kwa upande wake itahakikisha kuwepo kwa usimamizi makini wa utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka 2004/2005 ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, viongozi na watendaji katika ngazi ya Halmashauri za Wilaya wana nafasi kubwa na inabidi wawe mstari wa mbele kuwaelimisha wananchi kuhusu tafsiri sahihi ya marekebisho mbalimbali yaliyofanywa na Serikali kwenye mfumo wa kodi hasa kwenye sekta ya kilimo na leseni za biashara yanayolenga kuwaondolea kero, usumbufu na urasimu usio wa lazima ili watumie fursa hiyo kujiletea maendeleo na wasipotoshwe au kuyumbishwa na wajanja wachache. Ili kufikia malengo hayo ninawataka viongozi wote katika ngazi ya Wizara, Mikoa, Wilaya, Tarafa, Kata na Vijiji, wadau mbalimbali na wananchi wote kutekeleza kwa dhati sera na mikakati mbalimbali iliyoainishwa katika bajeti hii.

Aidha, Wakurugenzi wote wa Halmashauri za Miji na Wilaya wahakikishe kuwa wanayasaidia Mabaraza ya Halmashauri hizo kuoanisha bajeti zao na maamuzi yaliyotolewa kuhusu kodi mbalimbali. Yametokea baadhi ya malalamiko kuwa licha ya Serikali kufuta baadhi ya kodi zenye kero, bado wapo watendaji wachache kwenye baadhi ya Halmashauri wanaoendelea kutoza kodi hizo. Napenda kutumia fursa hii kutoa onyo kwa watendaji hao na kuwataka wazingatie na kusimamia kikamilifu utekelezaji wa maamuzi yote ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, maeneo yaliyopewa kipaumbele katika bajeti ya mwaka 2004/2005, ni yale yaliyoainishwa katika Mkakati wa Kupunguza Umaskini yakijumuisha sekta za elimu, afya, maji, kilimo, barabara, ardhi, Mahakama na mapambano dhidi ya UKIMWI. Aidha, mgao wa fedha pia umezingatia mahitaji muhimu yakiwemo kugharamia matayarisho ya Uchaguzi Mkuu ujao ikiwa ni pamoja na Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, mahitaji ya sekta ya nishati hasa umeme, hifadhi ya chakula na kuimarisha ulinzi na usalama. Kwa kuzingatia vipaumbele hivyo, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa bajeti kulingana na ilivyopitishwa na Bunge lako Tukufu.

Aidha, maeneo yote yaliyoonyesha udhaifu hasa katika ukusanyaji wa mapato na matumizi ya fedha za umma yataimarishwa. Nataka kueleza wazi kuwa kama tulivyoona sote, bajeti yetu haitoshelezi mahitaji yetu yote. Mahitaji ni makubwa kuliko uwezo, hivyo rasilimali hizo chache zitumike kwa uangalifu na umakini mkubwa. Nguvu za wananchi zisaidiane na rasilimali hizi katika kutekeleza baadhi ya majukumu kwa kadri inavyowezekana. Hivyo, ushirikishwaji wa umma ni nyenzo muhimu na ya lazima katika juhudi zetu za kutekeleza bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bajeti ya mwaka 2004/2005, ni ya tisa tangu Serikali ya Awamu ya Tatu iingie madarakani mwezi Novemba, mwaka 1995. Katika kipindi hicho chote kilichopita, tumeshuhudia mfululizo wa bajeti nzuri na makini, kama hii ya mwaka huu, za kutekeleza Ilani za Uchaguzi ya CCM na jitihada za Serikali zilizolenga katika marekebisho ya uchumi, kupambana na umaskini, kuboresha huduma za jamii na kupambana na kero mbalimbali. Mipango na bajeti zote hizo imeandaliwa na kutekelezwa chini ya uongozi imara na shupavu wa Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Benjamin William Mkapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kufuatia utekelezaji thabiti wa sera sahihi, mipango endelevu na bajeti hizi zinazolenga kuimarisha uchumi, tumepata mafanikio makubwa ya kisiasa, kijamii na kiuchumi katika kipindi cha miaka takriban tisa iliyopita. Katika kuhitimisha kipindi cha uongozi wa Rais Mkapa, Serikali itaendeleza misingi imara na matakwa ya kuimarisha uchumi tulivu, endelevu na unaokua mwaka hadi mwaka. Azma hii ya Serikali itawezesha uongozi wa Serikali itakayoingia madarakani mwezi Novemba 2005 kukabidhiwa uchumi ulio imara zaidi na mipango thabiti inayolenga katika kuboresha maslahi na maendeleo ya wananchi wetu. Aidha, Serikali itaendelea kuweka mazingira mazuri kwa uzalishaji hasa katika shughuli muhimu kama kilimo, uwekezaji na kukuza biashara ili kuuza bidhaa nyingi zaidi nje. Huduma za jamii nazo zitaendelea

kuboreshwa, ajira kuongezwa na uchumi kujitegemea zaidi ili kuondoa umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki cha Awamu ya Tatu ni dhahiri misingi mikuu ya uchumi *(Macro-Economic Fundamentals)* siyo tu imeimarika bali pia imetulizana. Uchumi unakua vizuri, mfumuko wa bei umedhibitiwa, mapato ya Serikali yameongezeka na kadhalika. Lakini bado utasikia malalamiko kuwa Serikali hii haijawasaidia wananchi kuondokana na umaskini na badala yake matajiri wachache ndiyo wanaoneemeka. Nataka nieleze kuwa katika uchumi wa soko unaokua, huo ni mpito wa kawaida. Katika mpito huo watu watapishana kwa ujuzi katika biashara, watu watapishana katika umakini wa kupata mitaji na kubwa kuliko yote, watapishana katika kuthubutu kuingia katika eneo wasilolijua. Katika mazingira hayo, kazi ya Serikali ni kulea mazingira ya uchumi ili yawe yanayotoa fursa hizo kwa wote, kuwaruhusu watu kutumia vipaji vyao, kuhakikisha kodi zinalipwa na kuzitumia kwa manufaa ya wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo ndivyo tulivyojitahidi kufanya nchini, tumejenga misingi imara ya uchumi na kutengeneza fursa nyingi za wananchi kujikwamua kiuchumi. Kama ilivyo kwa wengine, nchini mwetu wale waliokuwa ama na ujuzi katika biashara au uwezo wa kupata mitaji na kuthubutu kujitosa, wengi wao wamefanikiwa. Wale wasiokuwa na nyenzo hizo, hawakufanikiwa na kwa bahati mbaya ndiyo walio wengi. Lakini katika hali hiyo, Serikali hutekeleza wajibu wake kwa kuhakikisha kuwa hata wale walioachwa nyuma wanafaidi matunda ya nchi. Nchini mwetu tumefanya mengi ili kumpatia ahueni yule mwananchi wa kawaida kwa njia mbalimbali. Mifano michache ni kama ifuatavyo:

- Kuondoa kodi na ushuru mbalimbali ambazo zilionekana ama ni usumbufu kwa wananchi ama kikwazo kwa maendeleo. Mifano ni kodi ya maendeleo, ushuru mbalimbali wa mifugo, ushuru wa bidhaa ndogondogo na kadhalika. Misamaha hii imewezekana kwa kutoa fedha kwa wenye nazo kwa njia ya kodi na kuwapa wasionazo kwa njia ya kugharimia maendeleo yao. *(Makofi)*

- Uboreshaji wa elimu ambapo tuna miradi miwili sasa ya MMEM na MMES. Katika kuboresha elimu kwa shule za msingi, Serikali imeondoa ada na michango mbalimbali inayomlenga mzazi mwenye mtoto shuleni. *(Makofi)*

Kwa upande wa MMES, ada za shule za sekondari za kutwa ambazo ndizo nyingi zimepunguzwa na hata shule za binafsi ambazo watoto wa Watanzania wengi wanasoma humo, nazo zinafaidika katika mpango huu. Lakini miradi hii inagharimia maeneo mengine ya elimu kama ujenzi wa majengo, ununuzi wa samani, ukarabati wa majengo na kadhalika, kazi ambazo ingebidi wazazi wachange fedha zao ili kutekeleza hayo. Lengo la haya yote ni kumpunguzia mwananchi wa kawaida mzigo katika maisha yake.

- Huduma za afya nazo zimeboreshwa sana na baadhi ya makundi ya jamii hupatiwa huduma bure kama wazee wasio na uwezo, watoto wadogo na akinamama

wajawazito wanaojifungua. Hata wale wanaolipia huduma za matibabu, hulipia gharama za kuchangia na Serikali. Hii ni kumpatia ahueni mwananchi wa kawaida. *(Makofi)*

- Huduma zingine kama za maji na za barabara nazo zimeboreshwa sana na wananchi wote wanafaidika. Fedha zinazotumika zinatokana na mafanikio katika uchumi wetu kwa kukusanya kodi. *(Makofi)*

- Kwa upande wa wafanyabiashara, sasa leseni zitatozwa mara moja tu katika uhai wa biashara na viwango vimepunguzwa sana.

- Kwa upande wa watumishi, mishahara tunajua haitoshelezi mahitaji. Lakini mshahara wa kima cha chini umepanda kutoka shilingi 17,500/= kwa mwezi mwaka 1995/96 hadi shilingi 60,000/= kwa mwezi hivi sasa. Hii nayo ni kumpatia ahueni mfanyakazi wa ngazi ya chini.

- Kwa upande wa kilimo, kodi zote za Serikali Kuu zimeondolewa katika mazao, zana na pembejeo na tumeanza japo kwa kiwango kidogo kutoa ruzuku katika baadhi ya pembejeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeweza kuendelea kutoa mifano mingi zaidi. La muhimu ni kuwa katika uwezo wake mdogo, Serikali imejitahidi sana kuachia uchumi ukue na kutumia matunda ya ukuaji huo kwa faida ya wengi hasa watu wa kawaida.

Hili linawezekana tu kama kuna walipa kodi na kodi hiyo inakusanywa. Hivyo kusema huko kukua kwa uchumi hakujamsaidia mwananchi wa kawaida siyo kweli. Unafuu huo unaopatikana ni kwa sababu kuna waliofanikiwa na wanatozwa kodi inayotumika kutoa unafuu nilioueleza kwa walio wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya jumla, napenda sasa nigusie maeneo maalum machache. Eneo la kwanza ni lile la usimamizi wa fedha katika Halmashauri zetu. Hili ni eneo linalohitaji usimamizi wa karibu kutoka Baraza la Madiwani na viongozi mbalimbali wa Serikali. Bado Serikali itaendelea kupeleka fedha za ujenzi wa barabara kama inavyofanya sasa, fedha za huduma za afya na miradi mingineyo.

Aidha, fedha za elimu kwa mradi wa MMEM zitaendelea kutolewa na sasa tutakuwa na fedha zingine za mradi wa MMES. Shabaha kuu ya mpango wa MMES ni kuongeza idadi vijana wa Tanzania wanaosoma na kuhitimu kutoka 345,000 mwaka 2003 hadi milioni mbili mwaka 2010.

Natoa wito, kwa mara nyingine tena kwa wananchi kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa mpango huu ili kuwezesha vijana wetu wengi wa kike na kiume wanaohitimu na kufaulu elimu ya msingi kupata nafasi ya kujiunga na elimu ya sekondari. Aidha, kwa maeneo yenye shule za sekondari tayari, lakini zina upungufu wa wanafunzi, viongozi wa Wilaya wachukue hatua za kuondoa vikwazo vinavyokwamisha

ongezeko la idadi ya wanafunzi katika shule hizo. Kwa mfano, ujenzi wa hosteli, hususan kwa ajili ya watoto wa kike, nyumba za walimu, maabara na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni kero mbalimbali zinazowakabili wananchi wetu. Kwa maendeleo ya nchi yoyote suala la utawala bora ni la msingi sana. Ili wananchi wafanye kazi zao bila woga wala hofu, ni lazima kuwe na mazingira ya utulivu na ya amani. Ili tuweze kuwavutia wawekezaji wa nje na ndani ni lazima tuwe na mazingira ya amani na utulivu na mazingira ya utendaji wenye haki usiogubikwa na rushwa au maonevu mengineyo.

Ni dhahiri katika nchi yetu kama ilivyo kwa nchi zingine zenye mazingira kama yetu, bado kuna matatizo ya ujambazi na wizi wa kutumia silaha. Baadhi ya sababu za hali hii zinajulikana, lakini ninataka kuwahakikishia wananchi wetu kuwa Serikali inafanya kila liwezekanalo kupambana na matatizo haya. Jeshi la Polisi litaendelea kuimarishwa ili kukabili hali hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa tatizo la rushwa, juhudi nyingi zinaendelea kutekelezwa katika kupambana na ovu hili. Tarehe 17 Juni, 2004 Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais anayesimamia Utawala Bora, Mheshimiwa Wilson Masilingi, aliwasilisha maelezo ya Serikali kuhusu kazi kubwa iliyofanywa na inayoendelea kufanywa na Serikali katika kuimarisha utawala bora na vita dhidi ya rushwa. Ni kweli kuwa pamoja na juhudi hiyo ya Serikali, bado rushwa ni kero kwa wananchi wetu.

Hata hivyo, kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri, nchi yetu ni miongoni mwa nchi bora katika Bara la Afrika katika mapambano dhidi ya rushwa. Tumepiga hatua kubwa katika kuweka misingi ya utawala bora pamoja na taasisi za kusimamia utekelezaji wake. Bado tunahitaji kuwaelimisha na kuwahimiza wananchi kushiriki kikamilifu katika kulinda na kusimamia utekelezaji wa sheria na maamuzi mengine yenye lengo la kuimarisha utawala bora nchini.

Serikali itaendelea kuboresha utendaji kazi katika ngazi zote hizi ikiwa ni pamoja na kusisitiza uwajibikaji zaidi ili wananchi waweze kupata huduma bila bughudha au kuzungushwa.

Mheshimiwa Spika, ili tuendeleze kazi nzuri tunayoendelea kuifanya pamoja na kusimamia utekelezaji wa mikakati mbalimbali ya Kiwizara, Kitaasisi na Kimkoa ya kupambana na rushwa, Wakuu wa Wilaya hawana budi kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa utendaji kazi wa Watendaji wote walio chini yao ikiwa ni pamoja na kukutana na wananchi ili waweze kutoa kero zao na ziweze kutatuliwa.

Aidha, natoa wito maalum kwa wananchi kutumia kikamilifu Ofisi za Taasisi ya Kuzuia Rushwa zilizofunguliwa na zitakazofunguliwa kwenye Wilaya zote nchini. Vita dhidi ya rushwa ni vya kudumu hadi ushindi upatikane na lazima sote tushiriki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mkutano huu Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia kwa uchungu sana tatizo la upatikanaji na usambazaji wa nishati ya

umeme kwenye maeneo mbalimbali nchini. Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000 ibara 51 (iii) inasema:

"CCM katika kipindi hiki cha 2000-2005 itahimiza Serikali zake: Kutoa kipaumbele katika usambazaji wa umeme katika Miji Mikuu ya Wilaya iliyobaki, Miji Midogo ambayo ni Makao Makuu ya Majimbo ya uchaguzi na Vijiji hasa kule ambako gridi ya Taifa inapita". *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nirudie sehemu hiyo: "CCM katika kipindi hiki cha 2000-2005, itahimiza Serikali zake: Kutoa kipaumbele katika usambazaji wa umeme katika Miji Mikuu ya Wilaya iliyobaki, Miji Midogo ambayo ni Makao Makuu ya Majimbo ya Uchaguzi na Vijiji hasa kule ambako *Grid* ya Taifa inapita". *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, CCM haikusema Miji yote ya Wilaya itakuwa imepata umeme bali juhudi zitaelekezwa huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina imani Waheshimiwa Wabunge wanakubaliana nami kuwa japo hatujakamilisha kazi hiyo, lakini juhudi kubwa zimeelekezwa huko. Hata hivyo, juhudi hizo ziliathiriwa sana na hali ya ukame iliyoikumba nchi yetu ambapo imebidi fedha nyingi zitumike katika kuzalisha umeme badala ya usambazaji wake. Kama hili lisingefanyika, madhara kwa uchumi wetu yangelikuwa makubwa sana. Hata hivyo, kufikishwa kwa umeme katika makao makuu ya wilaya 8 na kuwepo kwa mpango unaotekelezwa hivi sasa wa kufikisha umeme katika makao makuu mengine 6 ifikapo mwaka 2005 ni ishara dhahiri ya dhamira ya Serikali kutekeleza Ilani hiyo ya CCM. *(Makofi)*

Aidha, yapo maeneo yenye matatizo maalum, kama vile Makao Makuu ya Mikoa ya Kigoma, Lindi na Mtwara ambayo Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Umeme nchini itaendelea kuchukua hatua za dharura na za muda mrefu kuhakikisha umeme wa uhakika unapatikana. Serikali inatambua umuhimu wa nishati hii kwa maendeleo ya wananchi. Ninataka kuwahakikishia wananchi wa maeneo yale yasiyo na umeme au yasiyo na umeme wa uhakika, kuwa kila juhudi itafanywa na Serikali kutatua tatizo hilo kutegemeana na upatikanaji wa rasilimali zinazohitajika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi za Serikali kwa kushirikiana na wadau wetu wa maendeleo katika kusambaza umeme wa gridi ya Taifa, ni vyema tuendelee kutoa msukumo katika kuendeleza na kueneza nishati mbadala. Hivi sasa upo uharibifu mkubwa wa mazingira unaotokana na kukata miti kwa ajili ya mkaa ambao matumizi yake yanaongezeka kwa kasi sana, hususan mijini. Kwa hiyo, tunayo kazi kubwa ya kueneza matumizi ya nishati mbadala kama vile nishati ya jua (umemenuru), upepo, n.k. Uharibifu wa mazingira unatokana pia na shughuli zingine za binadamu kama kukata misitu, kuchoma moto ovyo mbuga, kilimo na ufugaji usiofuata misingi ya ufugaji bora.

Katika siku za karibuni Serikali imechukua hatua za kinidhamu dhidi ya watendaji wachache wa Serikali waliokiuka taratibu katika Idara ya Misitu. Misitu ni raslimali muhimu sana katika hifadhi ya mazingira. Tusipoweza kusimamia sheria,

kanuni na taratibu zinazolinda na kuhifadhi misitu yetu, itaharibiwa na kuangamizwa kabisa na baadhi ya wale wachache ambao wanatanguliza maslahi binafsi mbele kuliko yale ya Taifa. Ni wajibu wa viongozi, wataalamu na wananchi katika ngazi zote kushirikiana ili tuweze kudhibiti uharibifu wa mazingira, uchomaji moto ovyo misitu na uvunaji holela wa mazao ya misitu. Vilevile tudhibiti uharibifu wa vyanzo vya maji, uchafuzi wa mazingira mijini, uvuvi haramu na ujangili. Maisha ya leo ya Watanzania na ya vizazi vijavyo yanategemea mazingira hai. Wito wangu leo kwa viongozi wa Serikali za Vijiji, Watendaji wa Kata, Makatibu Tarafa na Viongozi wa Wilaya ni kuwa suala la hifadhi ya vyanzo vya maji, misitu ya asili, upandaji na utunzaji wa miti na udhibiti wa uchomaji moto sio suala la kulipuuza tena. Mabadiliko ya hali ya hewa tunayoyashuhudia ni matokeo ya uharibifu wa mazingira unaoendelea nchini. Ni vyema basi sisi viongozi na wataalamu tuendelee kuelimishana na kuwahamasisha wananchi kuhusu hifadhi ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine muhimu sana kwa uchumi na maisha ya wananchi wetu ambalo Waheshimiwa Wabunge wamelizungumzia sana ni kilimo. Pamoja na umuhimu wake huo, kilimo chetu bado ni duni sana. Kinategemea mvua kwa sehemu kubwa, hakitumii pembejeo za kutosha, kinatumia teknolojia duni, kina tija ndogo na kwa sehemu kubwa huuza bidhaa ghafi ambazo bei zake ni duni sana katika masoko ya dunia. Ili kilimo chetu kibadilike, ni lazima tubadili baadhi au vyote vya vigezo hivyo.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imejaliwa kuwa na ardhi kubwa. Jumla ya eneo linalofaa kwa kilimo ni hekta 94 milioni na kati ya hizo hekta 44 milioni zinafaa kwa kilimo cha mazao na hekta 50 milioni zinafaa kwa ufugaji. Eneo linalotumika kwa kilimo hivi sasa ni hekta 10 milioni au asilimia 10.7 tu ya eneo lote au asilimia 23 ya eneo la kilimo cha mazao. Eneo linalofaa kwa umwagiliaji ni hekta 29.4 milioni, lakini linalotumika hivi sasa ni hekta 227,500 au asilimia 0.8. Uwezo wetu wa kilimo ni mkubwa na taarifa za kitaalam zinasema Tanzania tunaweza siyo kujilisha tu bali tukawa wauzaji wa nafaka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, biashara yetu ya mazao katika masoko ya dunia haina uhakika kwa sababu hatusindiki mazao. Aidha, ubora wa mazao yetu siyo wa kujivunia sana. Hivi sasa wakulima wetu wanalalamika sana bei za mazao yao zinaposhuka, na mara nyingi hudhani Serikali ndiyo husababisha hali hiyo. Ni vema wakulimawakafahamu kuwa Serikali siyo inayosababisha hayo na wala Serikali haina fedha za kufidia bei ya zao lolote inayoshuka katika masoko ya nje.

Ili kuboresha kilimo, ni muhimu mkulima kupata mahitaji yake muhimu kwa wakati muafaka na kwa utaratibu wa uhakika. Ili kufanikisha hili, ushirika wa wakulima ndiyo njia pekee. Napenda kusisitiza umuhimu wa kuanzisha na kuimarisha Ushirika wa Vyama vya Kuweka na Kukopa *(SACCOS)* kama nguvu pekee ya wakulima katika kuondokana na umaskini. Ni kwa njia ya ushirika na *SACCOS* wakulima wanaweza kuaminiwa kupata mikopo kutoka mabenki; ni kwa njia ya ushirika wakulima wanaweza kuagiza pembejeo kwa bei iliyo na unafuu zaidi kuliko kuwategemea wafanyabiashara binafsi, na ni kwa kutumia ushirika wakulima wanaweza kuuza mazao yao kwa bei ya

juu kuliko bei wanazopata sasa. Bila kuujenga na kuutetea ushirika ulio imara, itakuwa vigumu mno kwa wakulima wetu na wafugaji wetu, wavuvi na wazalishaji wadogo wa viwandani kuingia katika ushindani huria katika utandawazi wa kibiashara. Natoa wito kwa wadau wote wakiwemo Waheshimiwa Wabunge kujenga ushirika ulio imara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya kilimo ni pamoja na kujenga uwezo wetu wa ndani wa kusindika mazao. Wapo Watanzania wenzetu walioitikia wito wa Serikali wa kusindika mazao ya kilimo, mifugo na mazao mengine ya maliasili, kama vile nyuki na samaki. Wananchi hawa wengi wao wanazalisha bidhaa zao kwa ubora wa kimataifa. Napenda kutumia fursa hii kuwapongeza sana. Lakini hawa ni wachache mno ikilinganishwa na mazao ya kilimo na mifugo yanayouzwa bila kusindikwa au kuozea mashambani, hasa mazao ya matunda na mbogamboga. Natoa wito kwa Watanzania wengine, mtu mmoja mmoja, vikundi au ushirika, kuanzisha viwanda vidogo vidogo na vya kati vya usindikaji mazao ya kilimo, misitu, uvuvi na mifugo. Katika eneo hili nafasi bado ni kubwa na fursa ni nyingi. Hili ni mojawapo ya maeneo yaliyopewa kipaumbele katika uwekezaji na ina vivutio vingi. Aidha, Watanzania tujifunze kununua na kutumia bidhaa zetu wenyewe. Hivyo ndivyo tutakavyojenga uwezo wa soko la ndani.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha kisasa ni pamoja na matumizi ya kilimo kinachokubalika, matumizi ya mbegu bora, upandaji kwa nafasi inayotakiwa, matumizi ya pembejeo hasa mbolea na madawa ya kudhibiti visumbufu mimea na wadudu waharibifu, palizi kwa wakati unaotakiwa, uvunaji kwa wakati unaotakiwa, usindikaji kama upo, hifadhi ya mazao na hatimaye matumizi ya mwisho au kuuzwa sokoni. Haya yote ni mambo yanayohitaji utaalamu. Kwa mfano, madawa ya mimea ni sumu inayoweza kuua binadamu au mmea wenyewe yakitumiwa vibaya. Hata mbolea ikitumiwa vibaya ni hatari pia kwa binadamu, kwa udongo na kwa mimea. Hivyo ni vema wakulima wakachukua tahadhari kubwa katika matumizi ya pembejeo hizi. Tunazo taarifa nyingi za madawa yaliyoleta athari kwa binadamu na mimea. Aidha, pamewahi kutokeza makampuni au wakala wa madawa haya wakawauzia wakulima madawa yaliyokwisha nguvu yake. Hayo pia huleta madhara kwa mimea na binadamu. Kila mmoja sasa, mkulima na muuzaji wa madawa na pembejeo za kilimo wawe waangalifu na dosari hizi. Wizara ifuatilie kwa karibu uangalizi wa madawa na kuhakikisha ni yale tu yanayokubalika ndiyo yanayoingizwa nchini na kutumika na wakulima. Hatua kali zichukuliwe kwa wanaovunja sheria.

Mheshimiwa Spika, hali ya chakula nchini inatarajiwa kuwa nzuri katika mwaka wa 2004/2005 kama ilivyoelezwa kwa undani katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula. Kulingana na tathmini iliyofanywa na takwimu zilizopo tutajitosheleza kwa chakula. Tutakuwa na ziada katika baadhi ya mikoa, lakini kama sote tunavyofahamu ipo baadhi ya mikoa ambayo haikupata mvua za kutosha na hivyo kusababisha upungufu wa chakula katika baadhi ya maeneo ya mikoa hiyo. Mikoa hiyo ni Arusha, Kilimanjaro, Shinyanga, Pwani, Mtwara, Mwanza, Mara, Singida, Tabora, Dodoma, Tanga na Lindi. Kwa msingi huo, napenda kutoa wito maalum kwa wananchi katika maeneo yenye upungufu wa chakula kununua chakula kutoka maeneo yenye ziada. Aidha, wafanyabiashara wanunue chakula kutoka maeneo yenye ziada na kuuza katika

maeneo yenye upungufu. Ni vema ununuzi wa chakula kwa kaya zenye upungufu ufanywe sasa wakati bei ni za kuridhisha na chakula kinapatikana. Mikoa yenye mvua za vuli ijiandae kulima mazao yenye kukomaa haraka mvua za mwaka huu zitakapoanza na mabonde yenye kilimo cha kiangazi yalimwe kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, hali ya chakula katika nchi jirani za Afrika ya Mashariki na Kati sio ya kuridhisha na hivyo nchi hizo zinategemea kupata chakula kutoka nchi zenye ziada kama Tanzania. Hivi sasa nchi hizo zimeanza kununua kwa wingi chakula kutoka nchini mwetu. Katika hali hiyo ama ziada tuliyokuwa tumeipata itaondoka au labda hata imekwisha toka nje ya mipaka yetu. Hivyo, kama tahadhari, wananchi wenye upungufu wa chakula lazima wanunue chakula cha kutosha bila kusubiri na kukihifadhi kabla ya chakula hicho kuuzwa nje. Napenda nirudie kukariri maagizo ninayoyatoa kila mara kuhusu suala hili. Wakuu wa Wilaya wasimamie kikamilifu zoezi la hifadhi ya chakula katika ngazi ya kaya. Wananchi waelimishwe na kuhimizwa kuwa, hifadhi ya chakula cha kutosheleza kwa kaya ni suala lisiloepukika, hasa nyakati hizi ambapo hali ya hewa haitabiriki. Hifadhi ya Taifa ya Chakula *(SGR)* nayo iongeze kasi ya ununuzi wa chakula.

Mheshimiwa Spika, sera yetu ni biashara huria na tunapenda mkulima apate bei nzuri kwa mazao yake. Hii ndiyo maana tunaruhusu mazao yetu kusafirishwa bila kipingamizi ndani ya mipaka yetu. Nje ya mipaka yetu, utaratibu ni tofauti. Wale wanaotaka kusafirisha mahindi au biashara yoyote nje, lazima wawe na leseni halali za kufanya hivyo. Hivyo, Serikali inatoa agizo kuwa usafirishaji wa mazao ni huria ndani ya mipaka yetu. Usafirishaji wa mazao nje ya nchi ni marufuku bila leseni halali za biashara. Wakuu wa Mikoa ya mipakani wazingatie agizo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kilimo chetu kiko nyuma kwa sababu wale wenye uwezo wa kulima na kuonyesha mfano hawafanyi hivyo. Kuna wakati wanafunzi wahitimu wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine walimweleza Baba wa Taifa kuwa hakuna ajira Serikalini hivyo wao pamoja na kuwa na shahada zao itabidi wakalime. Marehemu Baba wa Taifa alionesha kufurahishwa kwake na maelezo hayo na kusema kuwa sasa labda kilimo cha Tanzania kitabadilika kama wataalam wenye shahada watakwenda kulima. Kwa vyovyote hilo siyo jibu walilolitarajia wahitimu wale na sidhani kama kuna aliyekwenda kulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi leo ningepata faraja sana kama kila Mheshimiwa Mbunge aliyeko hapa angekuwa na shamba zuri la mfano lisilopungua angalau ekari 1000. Hatuwezi kutetea kilimo kama shughuli ya msingi ya wananchi wakati sisi siyo waonyesha mfano. Wabunge na Watanzania wengi tuna rasilimali mfu *(dead capital)* nyingi ambazo tungezifufua, tungezitumia kupata fedha na kufungua mashamba ya kilimo au mifugo. Nyumba unayolala humo ndani unaweza ukaitumia ikakuzalishia mali nyingi. Ningefurahi sana kama sisi Wabunge tungeonyesha mfano kwani uwezo huo upo. Hilo lingetokea, nami ningelisema sasa kilimo cha Tanzania kitabadilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hali hii, sisi hatuonyeshi sana mfano sikushangaa hivi karibuni Bunge lako lilipopoteza muda muhimu wa Wabunge zaidi ya 200 kujadili kama

Waziri Mkuu ana shamba au anakodisha shamba Kibaigwa. Majadiliano yale yangetazamwa na Wabunge wa nchi nyingine wangetushangaa sana, pamoja na kwamba aliyekuwa anahoji alikuwa bila shaka na sababu zake binafsi.

Aidha, baadhi ya magazeti yamejitahidi sana kuandika juu ya shamba la Kibaigwa, shamba lisilozidi ekari 150 linalokodishwa na watu kadhaa akiwemo Frederick Sumaye kana kwamba ni jambo kubwa na muhimu sana. Labda Mheshimiwa Spika, kinachoendelea sasa ni hadithi ya zamani ya mzee fisi, kaka sungura na mzee kobe. *(Makofi/Kicheko)*

Mzee kobe alikuwa mlinzi wa shamba la mfalme wa wanyama kwa sababu ya tabia yake ya kutokulala. Sungura na mzee fisi wakashindwa kuiba shambani kwa mfalme kwa sababu ya ulinzi mkali wa mzee kobe. Wakaona dawa wamfitini mzee kobe kwa mfalme ati kuna mmea shambani ulikuwa umezaa tunda la dhahabu mzee kobe kalimeza. Kobe enzi hizo hakuwa na gamba. Wakampeleka kwa mfalme wakamwangusha chini na kuonyesha sehemu iliyotuna tumboni mwake kuwa ndiyo tunda hilo la dhahabu. Mzee kobe akalia sana kuwa jamani hicho ni kitovu changu lakini mzee fisi na sungura wakang’ang’ania kuwa ni tunda la dhahabu liko ndani.

Kabla hajapasuliwa, akatokea malaika wa wanyama na kumwuliza angependa nini cha mwisho kabla ya kifo chake. Mzee kobe akaomba kuwa kwa vile hana kosa, anaomba gamba la kujifichia ili hicho kisu kisimpate. Mzee kobe akapewa gamba lake. Mzee fisi na sungura waliposhindwa kumpasua, wakataka wamkate kichwa akakificha ndani, wakaamua wamkate miguu ili asiweze kulinda shamba na ashindwe kutembea, akaificha ndani. Hadi leo mzee kobe anatembea kwa uangalifu mkubwa akitunga sheria ili siku moja awashitaki mzee fisi na sungura kwa kumwonea. Naye fisi mpaka leo akimkuta mzee kobe lazima ampinduepindue akitafuta kama ataona kitovu, au kichwa au miguu ili aikate. Lakini *Inshallah* Mungu siyo Aziz wala Alfred, mzee kobe siyo alipona tu bali na gamba amelipata na analo mpaka leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika muda mfupi ujao kazi ya uandikishaji wa wananchi katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura itaanza. Waheshimiwa Wabunge tulipata fursa ya kuelimishwa kuhusu zoezi hilo na hatua ya maandalizi iliyofikiwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Kuanzishwa kwa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ni njia mojawapo ya kuimarisha na kuendeleza demokrasia katika mfumo wa vyama vingi hapa nchini kwa kuufanya uchaguzi uwe huru na wa haki. Mfumo huu mpya wa uandikishaji kwa kutumia Daftari la Kudumu la Wapiga Kura utasaidia kupunguza baadhi ya malalamiko ambayo yamekuwa yakijitokeza katika chaguzi zilizopita hasa kwa wale walioshindwa katika chaguzi hizo.

Vilevile, kuanzishwa kwa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kutapunguza gharama katika chaguzi zijazo. Kwa kawaida na kutokana na uzoefu wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, gharama za uandikishaji ndizo huwa kubwa katika zoezi la uchaguzi; uwe uchaguzi mkuu au chaguzi ndogo. Kwa hiyo, kuwepo kwa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kutapunguza kwa kiasi kikubwa gharama hizo hasa kwa chaguzi zinazofuatia. Kwa uhakika uandikishaji wa wapiga kura ni hatua muhimu katika uchaguzi, kwani

pasipokuwepo wapiga kura haiwezekani kuwa na uchaguzi. Umuhimu wa hatua hiyo ndiyo unaotiliwa maanani katika kuanzisha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Hivi sasa sote tunakubaliana kuhusu umuhimu wa Daftari hilo kwa maendeleo na ustawi wa demokrasia nchini mwetu. Mafanikio ya zoezi hilo yatategemea ushirikiano wa wadau wote katika kutoa elimu na kuwahamasisha Watanzania wote wenye umri wa kupiga kura wakajiandikishe mara muda utakapowadia katika maeneo yao.

Napenda kutoa wito kwa wananchi wote wenye sifa za kujiandikisha kuwa wapiga kura, kujitokeza kwa wingi kwenda kujiandikisha wakati Tume itakapotangaza kipindi cha kujiandikisha. Napenda kusisitiza kuwa hii itakuwa ni nafasi pekee ya kujiandikisha kwa ajili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani utakaofanyika mwaka 2005. Uchaguzi wa viongozi wa nchi yetu ni suala muhimu sana, kwani zoezi hilo ndilo linalowapa wananchi nafasi ya kutoa ridhaa yao kwa viongozi wanaowaona kuwa wana uwezo wa kuendeleza maslahi ya nchi yetu. Ni vyema sisi viongozi, hususan Waheshimiwa Wabunge tuwasaidie wananchi watambue kuwa wasipokuwa na kitambulisho cha mpiga kura hawataweza kupiga kura mwakani.

Aidha, mara wapatapo kadi za kuwatambulisha kama wapiga kura wazitunze kadi hizo, kwani hizo ndizo zitakazowawezesha kupiga kura mwakani na miaka mingine mingi ijayo inayofuatia. Wajibu wa viongozi wote tukiwepo sisi Waheshimiwa Wabunge ni kusaidiana na Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi. Napenda kutumia fursa hii kupongeza uongozi wa vyama vya *CUF,* CHADEMA na CCM kwa kukubali kushirikiana na Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika maandalizi ya Daftari hili. Wito wangu kwa wadau wengine wote ni kuwa, ni vyema watambue kuwa uandikishaji wapiga kura ni hatua muhimu katika uchaguzi na kwa hivyo wanalo jukumu la kushirikiana na Tume ya Taifa ya Uchaguzi ili tuweze kujenga misingi imara ya uchaguzi ulio huru na wa haki.

Mheshimiwa Spika, kama tulivyoelezwa katika mkutano huu, tutakuwa na Uchaguzi wa Viongozi wa Serikali za Vijiji, Mitaa na Vitongoji mwishoni mwa mwaka huu. Ngazi hizi za mamlaka ndizo zilizo karibu sana na Wananchi wetu. Ujenzi wa dhana ya demokrasia ni pamoja na kuwawezesha wananchi katika ngazi hizi kufanya maamuzi yanayohusu maendeleo yao. Kazi ya Serikali ni kuwawezesha tu wananchi kwa kutoa elimu na kuchangia katika rasilimali za fedha na vifaa ili kufanikisha uchaguzi huo. Idadi ya wananchi wanaoishi katika vitongoji ni ndogo inayowafanya wananchi kufahamiana sana kwani wanasaidiana na kushirikiana kwenye shughuli zao za maendeleo.

Kwa msingi huo, ni vyema wakaachiwa uhuru wa kufanya maamuzi yao. Kanuni za uchaguzi zilizotungwa zinawawezesha tu kufanya uchaguzi wao na kuondoa matatizo yasiyotarajiwa. Napenda kutoa wito maalumu kwa Waheshimiwa Wabunge na viongozi wa vyama vya siasa kushiriki katika kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa uchaguzi huu na kuwahamasisha wananchi kushiriki kikamilifu. Kama tunavyoelewa hivi sasa tunaelekeza fedha nyingi hususan za huduma za jamii katika ngazi za vijiji na mitaa, kwa hiyo ni vyema tupate viongozi madhubuti watakaoweza kutoa uongozi

utakaowahamasisha wananchi kuchangia nguvu zao na kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika ngazi hizo.

Mheshimiwa Spika, wakati natoa hoja ya kuliahirisha Bunge katika mkutano wa kumi na tano, nilieleza kuhusu joto la kisiasa linavyopanda nchini hivi sasa kutokana na kukaribia chaguzi hizi za Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu mwaka 2005. Hivi karibuni tumeanza kusikia matamshi mazito ya vitisho ambayo yana lengo la kupotosha ukweli ulivyo na hata matarajio ya wananchi walio wengi wapenda amani na maendeleo ya nchi yetu.

Ni kweli kuwa malengo ya chama cho chote cha siasa ni kushika dola. Hata hivyo, ni vyema ieleweke kuwa ridhaa ya kushika dola hutolewa na wananchi tu kupitia kura zao. Jukumu la vyama vya siasa hivi sasa ni kuwaelimisha wanachama wao na wananchi kwa ujumla watambue haki na wajibu wao katika chaguzi zinazokuja na kuwahamasisha washiriki kikamilifu katika hatua zote. Lugha ya vitisho haitusaidii katika kujenga mfumo wa demokrasia unaozingatia uvumilivu na utashi wa wananchi. Napenda kutoa wito kwa viongozi wa kisiasa nchini kujihadhari na kauli zenye kuchochea vurugu na machafuko.

Hata hivyo, napenda kuuhakikishia Umma wa Watanzania kuwa chama chenye ridhaa ya wananchi na kikapewa dola hadi baada ya matokeo ya Uchaguzi Mkuu mwaka 2005 ni Chama cha Mapinduzi na CCM kiliunda Serikali zake baada ya ridhaa hiyo. Moja ya jukumu kubwa la Serikali yoyote iliyopo madarakani ni kuhakikisha ulinzi na usalama wa uhai na mali za wananchi. Kwa msingi huo, Serikali zetu zote zitaendelea kuhakikisha kuwa tunakuwa na mazingira ya amani yatakayowawezesha wananchi kushiriki katika shughuli zote za uchumi, kijamii, kisiasa zikiwemo chaguzi mbalimbali. Ninaomba sana sote tutii Serikali na vyombo vyake na hakuna atakayesukumwa hata kidogo. Tusipotii, vyombo vya dola vitafanya kazi zao. Watanzania tuenzi amani na utulivu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ninapenda nilizungumzie ni jinsi lugha ya Kiswahili inavyokuwa lugha muhimu katika Bara la Afrika na katika baadhi ya sehemu duniani. Tanzania ni lazima tuone fahari kubwa kwa matokeo haya. Ninapenda kuwashukuru sana Ma-Rais wa Umoja wa Afrika kwa kukubali kukifanya Kiswahili kuwa lugha mojawapo rasmi ya kutumika katika mikutano ya umoja huo. Ninapenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Rais Mkapa na wenzake walioanza kukitumia Kiswahili katika vikao vya umoja huo. Kwa hatua hiyo muhimu sisi Watanzania, lazima tuwe msitari wa mbele katika kukienzi Kiswahili, kwanza kwa kukiboresha kadri inavyowezekana, kukitumia kadri inavyowezekana na kuwashawishi wengine wakitumie kadri inavyowezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matumaini yangu vilevile ni kuwa taasisi zetu muhimu kama Bunge lako Tukufu litakuwa msitari wa mbele katika kukienzi Kiswahili. Hata hivyo, ninapenda kusema kwa masikitiko makubwa kuwa Bunge lako ni moja ya taasisi inayovuruga uboreshaji wa Kiswahili. “Napenda nirudie sehemu hiyo, hata hivyo

napenda kusema kwa masikitiko makubwa kuwa lako ni moja ya taasisi inayovuruga uboreshaji wa Kiswahili”. *(Makofi/Kicheko)*

Ukisoma taarifa zetu za majadiliano ya Bunge *(Hansard)* utakuta lugha za mchanganyiko sana. Naomba nitoe mifano michache niliyoiona katika taarifa za majadiliano michache sana. kwa mfano, Mheshimiwa Mbunge anasema, Waziri u-*clean your house,* neno u-*clean* haliko katika lugha yoyote. *(Kicheko)*

Mwingine alisema ina-*confuse* madereva, neno ina-*confuse* haliko katika lugha yoyote. Mwingine amesema *they can afford* ku-*hire a tax consultant* na wanaweza waka-*afford* ku-*hire a lawyer,* maneno ku-*hire* na waka-*afford* ni lugha gani? *(Makofi/Kicheko)*

Mwingine akasema anapokuwa anam-*train employee* wake akaendelea kusema kuwa-*encourage* wale *employers* katika ku-*train staff* wao. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hii lugha haieleweki. Yako maneno mengi, utakuta maneno kama ku-*import Capital Goods, Multiple* leseni, mwingine amesema bajeti hii haina *vibrancy, economic growth* imekosekana. *(Kicheko)*

Mwingine amesema, Bajeti ime-*generalize* mambo, mwingine amesema: “*Wananchi they are making statement* ya kuwa hawaridhiki, kuna maneno mengi kama ku-*regulate,* una-*invest,* ku-*subsidize,* unapo-*balance,* ku-*challenge, TRA wange-consult,* na kadhalika. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa vurugu ya namna hii, anayetusikiliza kama anajua Kiingereza anatushangaa na kama anajua Kiswahilii pia anatushangaa. Kanuni zetu zinaruhusu lugha mbili tu Kiingereza na Kiswahili. Hii lugha ya tatu imetokea wapi? Hivyo sishangai niliposoma kwenye gazeti moja kuwa mtu mmoja alikuwa anahangaika kutafuta Kamusi ya *Kiswanglish* kwa sababu Bunge lilikuwa karibu kuanza mkutano wake. Tusipoangalia tutaanzisha lugha rasmi ya tatu iitwayo *Kiswanglish. (Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba Bunge lako Tukufu liungane na Watanzania wengine kutumia Kiswahili sanifu ili tuwe kitovu cha Kiswahili katika Afrika na dunia kwa jumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mkutano huu wa bajeti tangu mwanzo lilijitokeza tatizo kubwa la madai mbalimbali ya walimu. Naamini wapo pia watumishi wengine ambao siyo walimu wanaoidai Serikali. Kwa upande wa walimu tatizo limekuwa kubwa sana, hivyo tarehe 23 Juni, 2004 wakati nahitimisha Hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu niliahidi kulifuatilia jambo hili kwa njia zifuatazo:-

1. Kuagiza madai yaliyohakikiwa yalipwe kwa pamoja na mishahara ya mwezi Julai 2004. Taarifa nilizopewa ni kuwa madai yote yaliyofika Hazina na yameshakikiwa yamekwishalipwa. Walimu waliokuwa hawajaingizwa katika malipo ya kompyuta wengi wao wameingizwa tayari na waliobakia ambao taarifa zao zimekwishawasilishwa Hazina

wanaingizwa mwezi huu ili mishahara yao ya mwezi Agosti, ipatikane kwa njia hiyo. Hii ni kwa walimu wote wapya pamoja na walimu wanafunzi. *(Makofi)*

Aidha, kwa madai yale ambayo hayajafika Hazina, nimeunda *Task Force* inayoongozwa na Utumishi kuhakikisha madai hayo yanapatikana na kulipwa mara moja. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mimi nimesema Tume Ndogo *(Task Force)*. Ningesema nii-*task* labda ndiyo ingekuwa tatizo. *(Kicheko)*

2. Mheshimiwa Spika, niliagiza wakuu wa mikoa waunde tume za kufanya uchunguzi juu ya matatizo ya walimu katika Halmashauri katika mikoa yao na taarifa zao zifike ofisini kwa Waziri Mkuu siyo zaidi ya tarehe 31 Julai 2004. Nafurahi kutoa taarifa katika Bunge lako Tukufu kuwa Wakuu wa Mikoa wote walitekeleza agizo hilo na walileta taarifa zao wao wenyewe binafsi na kuziwasilisha tarehe 30 Julai 2004. Taarifa hizo zinafanyiwa uchambuzi. *(Makofi)*

3. Niliahidi kuunda tume ya kufuatilia matatizo ya walimu ili kuyatatua yaliyopo na kushauri namna ya kutoyarejea matatizo haya mara kwa mara. Tume hiyo itatembelea kwa kadri inavyowezekana Halmashauri zote na kubaini matatizo ya walimu. Lengo la tume ni kuisaidia Serikali na pia kuwasaidia walimu ili wasiendelee kupata matatizo haya.

Tume itakuwa na uhuru wa kuongea na walimu, wawakilishi wa walimu, viongozi wa Serikali na wadau wengine kama viongozi wa siasa na taasisi nyingine kwa kadri watakavyoona inafaa. Naomba tume hii ipewe ushirikiano kwa sababu siyo tume ya kufunga watu bali ni tume ya kutusaidia kupata ukweli ili kutatua tatizo.

Aidha, tume itaangalia taratibu zote ziwe za ajira, uwajibikaji, ujazaji fomu muhimu za taarifa ya ajira ya mtumishi na mchakato mzima hadi mwalimu anapopata mshahara wake. Tume itaangalia namna ya kuboresha mazingira ya jumla ya mwalimu, na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tume hiyo nimekwishaanza kuiunda na itaongozwa na Mheshimiwa Omar Shabaan Kwangw' ambaye ni mwalimu mzoefu na ni Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii. Wajumbe wengine wataarifiwa watakapoteuliwa. Kwa ajili ya ufinyu wa muda na ukubwa wa kazi hii, tume inapewa muda wa miezi miwili kukamilisha kazi hii. Hivyo, tume inaagizwa ikutane Dodoma, Ofisi ya Waziri Mkuu tarehe 18 Agosti 2004 ili ianze na kazi ya kupitia taarifa za Wakuu wa Mikoa na taarifa ya uhakiki wa madai ya walimu iliyofanywa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Matumaini yangu ni kuwa tume hii itatusaidia sana. Naitakia kazi njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijahitimisha kwa kukushukuru wewe, naomba nimpongeze sana Rais wetu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa kwa kazi kubwa anayoifanyia nchi yetu, Afrika na ulimwengu kwa jumla. Leo Tanzania inaheshimika

sana duniani kwa sababu ya juhudi zake. Hali ya uchumi wetu inaendelea kuwa nzuri kwa sababu ya juhudi na upeo wake. Katika kutambua mchango wake kimataifa, amekuwa mwenyekiti Mwenza wa Tume ya Kimataifa ya Masuala ya Kijamii kuhusu Utandawazi na ameteuliwa na Waziri Mkuu wa Uingereza kuwa katika Tume ya Afrika kuhusu kusukuma mbele maendeleo ya Afrika. Tunachoweza kumpa Mheshimiwa Mkapa ni asante kwa heshima aliyoiletea Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda vilevile kutumia fursa hii kumpongeza sana Mtanzania mwenzetu Ndugu Ali Mchumo kwa mafanikio makubwa yaliyomwezesha kuchaguliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko wa Umoja wa Mataifa unaoshughulikia Bidhaa za Kilimo *(Common Fund for Commodities).* Kuchaguliwa kwake kumeiletea nchi yetu heshima kubwa. Pamoja na kumtakia kazi njema, napenda kumhakikishia kuwa Watanzania tutamsaidia afanikishe kazi zake, lakini pia tutaitumia nafasi hiyo kwa manufaa ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shughuli za mkutano huu zilianza tangu tarehe 24 Mei 2004 wakati Vikao vya Kamati za Kudumu za Bunge lako Tukufu zilipoanza kazi ya kuchambua Bajeti na Mpango wa mwaka wa Serikali pamoja na makadirio ya matumizi ya Wizara mbalimbali. Tangu wakati huo umetuongoza kwa hekima na busara kubwa. Napenda kutumia fursa hii kukushukuru na kukupongeza sana kwa uongozi wako thabiti. Napenda vilevile nimshukuru Naibu Spika, Mheshimiwa Juma Jamaldin Akukweti, Mbunge wa Tunduru, kwa kukupa msaada mkubwa katika kuliongoza Bunge hili. Nawapongeza Wenyeviti wetu maarufu, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mbunge wa Mbozi Magharibi na Mheshimiwa Anne S. Makinda, Mbunge wa Njombe Kusini kwa msaada mkubwa waliokupatia wewe Mheshimiwa Spika na Naibu Spika katika kuongoza mkutano huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, wameweza kutekeleza majukumu yao kutokana na mipango mizuri na ratiba nzuri iliyopangwa na Kamati ya Uongozi ya Bunge na huduma mbalimbali zilizotolewa na watumishi wa Ofisi ya Bunge. Napenda kuishukuru Kamati nzima ya Uongozi ikisaidiana na Tume ya Bunge kwa mipango hiyo mizuri na kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Kipenka M. Mussa, Katibu wa Bunge na Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya ya kutoa huduma mbalimbali kwa Waheshimiwa Wabunge. Aidha, uwezo wa Serikali kuwasilisha hoja zote ndani ya Bunge lako Tukufu kwa kuzingatia ratiba kumewezeshwa na watumishi wa Serikali na taasisi zake zote chini ya uongozi wa Katibu Mkuu Kiongozi, Bwana Marten Lumbanga. Napenda kuwashukuru nyote kwa kazi yao nzuri.

Mheshimiwa Spika, vyombo vya habari vimefanya kazi kubwa na nzuri ya kuwafikishia habari wananchi kuhusu majadiliano na hatimaye maamuzi ya Bunge lako Tukufu. Matangazo ya Televisheni yamekuwa na mvuto wa kipekee, kwani wakati wote yalionyesha moja kwa moja mambo yalivyokuwa yanaendelea ndani ya ukumbi huu wa Bunge. Napenda kuwashukuru wamiliki na viongozi wote wa vyombo vyote vya habari nchini pamoja na waandishi wote wa habari waliowezesha wananchi kufahamu yaliyokuwa yanaendelea katika kipindi chote cha mkutano huu.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge, wote kwa michango yao ya mawazo wakati wa majadiliano na hatimaye kwenye maamuzi mbalimbali yaliyofikiwa. Napenda kuwahakikishia kuwa yote mliyoyaeleza tumeyasikia. Yale yaliyo tayari ndani ya mpango wa bajeti ya Serikali tutayasimamia ili yaweze kutekelezwa. Ahadi zilizotolewa na ambazo zinahitaji utafiti, uchambuzi zaidi na fedha zitafanyiwa kazi na pale itakapowezekana kuwekwa katika mpango wa mwaka ujao, ili tuweze kupiga hatua katika kupunguza kero mbalimbali zinazokwamisha kasi ya maendeleo yetu. Waheshimiwa Wabunge wenzangu huu ni mkutano wa kumi na sita. Mkutano mwingine wa bajeti kama huu ndiyo mwisho wa uhai wa Bunge hili. *(Makofi/Kicheko)*

Najua hivi sasa majimboni kuna nini. Joto limepanda na siku zitazidi kuwa fupi kadiri siku zinavyozidi kusogea. Lakini jambo la muhimu tukashirikiane na wananchi kusimamia maendeleo yao. Kama hukuwasahau unawawakilisha nao watakukumbuka.

Napenda kuwatakia safari njema mnaporejea kwenye majimbo yenu na nawaomba mshirikiane na uongozi wa Wilaya na Mikoa yenu katika kusimamia utekelezaji wa maamuzi yote muhimu tuliyokubaliana ndani ya mkutano huu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba kutoa hoja kuwa Bunge lako Tukufu sasa liahirishwe hadi tarehe 2 Novemba, 2004 saa 3.00 asubuhi litakapokutana hapa Mjini Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Kabla sijawahoji ningependa kutoa taarifa moja ambayo nafikiri ni vizuri Waheshimiwa Wabunge, mkawa nayo mnapoondoka Dodoma kesho. Kama mnavyojua kazi ya Mwenyezi Mungu, aliyoifanya wakati tukiwa hapa imetunyang'anya wenzetu wawili. Kwa maana hiyo, sasa kuna nafasi wazi katika Majimbo mawili ya Uchaguzi.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano kifungu 76 (2) inasema kutakuwa na Uchaguzi wa Mbunge katika jimbo la Uchaguzi ikiwa kiti cha Mbunge yeyote aliyechaguliwa kuwakilisha Jimbo hilo kitakuwa wazi kwa sababu yoyote kwa matakwa ya Katiba. Sheria ya uchaguzi yenyewe kifungu cha 48 (3) kinamtaka Spika, Kiti cha Bunge kinapokuwa wazi Spika. amwandikie Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi kumjulisha kwamba kuna kiti wazi ndani ya Bunge na barua hiyo ya Spika ndiyo inakuwa idhini kwa Tume ya Uchaguzi kuanza kufanya maandalizi ya Chaguzi ndogo.

Kifungu cha 3 cha Ibara ya 76 kinasema bila kujali masharti ya ibara hii yaliyotangulia kama hilo nililosoma ifahamike kwamba ikiwa tarehe ya kuvunjwa Bunge imetangazwa au inafahamika basi uchaguzi wa namna yaani Uchaguzi mdogo hautafanywa katika kipindi chote cha miezi 12 ya nyuma ikihesabiwa kuanzia tarehe ya kuvunjwa Bunge kama inafahamika.

Sasa katika utaratibu wetu tuliuzoea Mheshimiwa Rais, huwa anavunja Bunge mara baada ya mkutano wa Bajeti wa mwaka wa tano wa maisha ya Bunge. Kwa hiyo, kutokana na mazoea hayo tunaweza kufahamu kwamba mnamo mwezi wa nane wa mwaka ujao kwa tarehe atakayoamua mwenyewe atalivunja Bunge hili.

Kwa kujua kwamba Katiba inazuia uchaguzi mdogo usifanyike katika miezi 12 kabla ya kuvunjwa Bunge na huu ni mwezi wa nane na kama Bunge litavunjwa mwezi wa nane mwaka kesho, basi kwa hiyo, Katiba hairuhusu Uchaguzi mdogo ufanyike kwa sababu hiyo sikusudii kumwandikia Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi, kumjulisha kwamba kuna nafasi wazi humu.

Kwa hiyo, ni vizuri Waheshimiwa Wabunge na majimbo yale ambayo yalipata matatizo hayo wajue kwamba hapatakuwa na Uchaguzi mdogo tutasubiri Uchaguzi Mkuu wa mwaka kesho Oktoba, 2005 ndipo wachaguliwe Wabunge wa majimbo haya pamoja na Wabunge wengine Tanzania nzima. *(Makofi)*

Sasa baada ya maelezo hayo naomba tuamue hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu ya Kuahirisha Bunge mpaka tarehe 2 Novemba, 2004. Hoja ya kwenda kujifagilia kwenye Majimbo yetu. Wanaokubaliana nami waseme *"Ndiyo"* na wanaotaka kutu-*confuse* waseme "Siyo".

Nafikiri hao "Siyo" wanaogopa kwenda kwenye Majimbo yao ya Uchaguzi.

Waheshimiwa Wabunge, mpaka hapo Bunge linaahirishwa hadi tarehe 2 Novemba, 2004 saa tatu asubuhi katika ukumbi huu huu wa Bunge hapa Dodoma. *(Makofi/Kicheko)*

*(Saa 12.23 Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumanne, tarehe 2 Novemba, 2004 saa 3.00 asubuhi)*